Nipashe
Jumamosi Agosti 29, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580323
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




UKURASA 11



## Wagombea wanne wachukua fomu kugombea urais Zanzibar

UKURASA 3

# KITIMTIMU

**CHADEMA** yaanza rasmi mbio za uchaguzi, yaomba kurudishwa wagombea wote walioenguliwa, TBC watimuliwa mkutanoni, NEC yaanika 18 waliopita bila kupingwa...

*Endelea ukurasa. 2*





Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akiwapungia mkono wanachama, wafuasi na mashabiki wa chama hicho, wakati wa uzinduzi wa kampeni za uchaguzi mkuu, katika viwanja vya Mbagala Zakhem, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## MCHUNGAJI MATATANI KWA MADAI YA UPATU

UKURASA 4

## CCM yatamba kuishangaza dunia uzinduzi kampeni leo

UKURASA 2



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

MICHEZO SIMBA QUEENS YASAJILI NYOTA WA YANGA PRINCESS, MLANDIZI UK.23
MAONI, KATUNI UK.6

# CCM yatamba kuishangaza dunia

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema leo kinatarajia kuishangaza dunia wakati kikizindua kampeni za uchaguzi mkuu wa urais, ubunge na udiwani katika Uwanja wa Jamhuri, jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, alisema utakuwa uzinduzi wa aina yake ambao haujawahi kufanywa na chama chochote.

"Uwanja wa Jamhuri tutakuwa na jambo letu kesho (leo). Tutaisimamisha dunia. Halitakuwa jambo la kubahatisha, utakuwa uzinduzi babu kubwa," alisema Polepole na kuongeza:

"Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipanga Agosti 26 kuwa ni siku ya kuanza kwa kampeni, lakini sisi tukajipa siku tatu za kuandaa mitambo yetu, sasa siku yenyewe imefika. Ratiba itaanza saa moja asubuhi hadi saa 12 jioni.

"Kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana kutakuwa na ubunifu wa hali ya juu kutoka kwa wasanii wakieleza mafanikio ya Rais John Magufuli."

Polepole alisema kuanzia saa 7:00 mchana shughuli rasmi za kampeni zitaanza na kwamba wanatarajia uwanja kufurika, hivyo kutafungwa Televisheni nje ya uwanja ili kuwawezesha Watanzania watakaoshindwa kuingia uwanjani kutazama.

"Matangazo yatakuwa mubashara kwa vyombo mbalimbali, mgombea wa CCM Rais John Magufuli ataelezea mafanikio katika miaka mitano, kuueleza ulimwengu mambo mazuri yaliyofanyika, changamoto tulizokutana nazo pamoja na mambo makubwa yaliyofanyika na yanayotarajia kufanyika," alisema.

Aidha, Polepole alisema katika uzinduzi huo, wasanii mbalimbali wanatarajia kutumbuiza wakiwamo Diamond, Ali Kiba, Harmonize, Masanja, Hamza Kalala, Mrisho Mpoto, Lavalava, Beka Flavor, Shilole, G-Nako, Nandi, Maua Sama na Joti.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma limesema limejipanga vyema kuhakikisha uzinduzi huo unafanyika kwa usalama.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Gilles Muroto, alisema wamejipanga kuhakikisha amani na usalama vinakuwapo kwenye kampeni hizo.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, akikagua ajali ya basi la abiria la NBS lenye namba za usajili T 571 BPZ, baada ya kugongana na gari dogo katika eneo ya Nyasamba, wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga, juzi na kusababisha vifo vya watu watano papo hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ni kitimtimu

**Waandishi Wetu**

NI kitimtimu! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya jana baadhi ya vyama vya siasa kuanza rasmi kampeni za kuusaka urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu.

Wakati chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kikitarajia kuzindua rasmi kampeni zake za urais leo jijini Dodoma, chama kikuu cha upinzani nchini kwa sasa, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kilizindua rasmi kampeni zake jijini Dar es Salaam jana.

Katika uzinduzi huo uliofanyika kwenye Viwanja wa Mbagala Zakhem jijini, tofauti na ilivyotarajiwa kwamba kingeanza kunadi sera na ilani ya uchaguzi wa mwaka huu, chama hicho kilitoka na tamko la kushinikiza kurudishwa kwa wagombea wake wote na wa vyama vingine walioenguliwa kuwania nafasi za ubunge na udiwani katika maeneo mbalimbali nchini.

Vilevile, uongozi wa juu wa chama hicho, uliwafukuza waandishi wa habari wa Televisheni ya Taifa (TBC) waliokuwa wakirusha moja kwa moja matangazo ya uzinduzi wa kampeni hizo kwa tuhuma za kuendesha mchezo mchafu dhidi ya chama hicho kilichoshika nafasi ya pili katika mbio za urais mwaka 2015.

**ILIVYOKUWA MBAGALA**

Maelfu ya wanachama na wafuasi wa CHADEMA walijitokeza kwenye ufunguzi wa kampeni hizo kwenye viwaja vya Mbagala Zakhiem, mgombea urais kupitia chama hicho, Tundu Lissu, akitoka makao makuu ya chama Kinondoni saa 6:36 mchana kwa msafara ambao ulipita Posta ya zamani kuelekea Kigamboni kwa kutumia kivuko na kupokewa na wanachama wa chama hicho ambao waliungana naye.

Msafara huo ulipita Mji Mwema na kutokea Daraja la Kigamboni ambako ulisimama kwa muda na baadaye ulipita Barabara ya Kilwa na kuingia uwanjani huko saa 8:16 mchana.

Katika msafara huo, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, hakuwa sehemu yake, lakini baadaye aliungana na wagombea wa chama hicho kwenye mkutano wa kampeni na alipopata fursa ya kuzungumza na wananchi, alitoa robo saa kwa waandishi wa habari wa TBC kuondoa mitambo yao iliyokuwa uwanjani huko kwa madai kuwa walikuwa wanakatakata matangazo ya kampeni zao.

Baada ya kutolewa kwa tamko hilo, baadhi ya wananchi waliokuwa wamejitokeza, walianza kuondoka uwanjani huko, lakini hali ilitulia baada ya Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi kwa watendaji hao wa TBC. Kituo hicho cha luninga kilisitisha matangazo hayo ya moja kwa moja baada ya tamko hilo la Mbowe.

Mbali na kuwafukuza TBC, Mbowe alisema kuwa kamwe hawataondoka kwenye uchaguzi huo, lakini akasisitiza kuwa msimamo wao kuhusu suala hilo ulitarajiwa kutolewa baadaye na mgombea wao wa kiti cha urais, Lissu.

Baada ya kupewa fursa ya kuzungumza, Lissu alisema wamezungumza na chama cha ACT-Wazalendo, ambacho wamekuwa katika mjadala wa kushirikiana, kuhusu kuenguliwa kwa wagombea wao Tanzania Bara na Zanzibar.

Lissu pia alisema ameahirisha kusoma hotuba yake aliyoiandaa yenye kurasa 24 kutokana na yanayoendelea ya kuenguliwa kwa wagombea wao, akidokeza kuwa alikuwa amepanga kutoa muhtasari wa namna alivyopigwa risasi na safari yake ya matibabu ya kibingwa Nairobi na Ubelgiji.

Mtaalamu huyo wa sheria alisema aliweka wazi kuwa alisafirishwa kwenda Nairobi kupata matibabu kwa msaada wa mbunge wa CCM ambaye hata hivyo, hakumtaja kwa jina.

Lissu alisema haoni hajaa ya kuanza kuomba kura na kunadi sera za chama hicho kuelekea uchaguzi huo ilhali idadi kubwa ya wagombea wao wa nafasi za ubunge na udiwani imefyekwa.

Alibainisha kuwa chama chao kilikuwa kimesimamisha wagombea wa udiwani 3,754 nchi nzima, lakini hadi jana, wagombea 1,020 walikuwa wameenguliwa huku wagombea 53 kati ya 244 wa nafasi za ubunge nao wakikatwa kutokana na sababu mbalimbali ambazo alidai ni za kionevu.

Lissu alidai kuwa chama cha ACT-Wazalendo nacho kimekumbwa na baa hilo la wagombea kuenguliwa, akibainisha kuwa hadi jana, wagombea wake 47 wa ubunge, wakiwamo 16 kati ya 18 wa majimbo yote ya Pemba, walikuwa wamekatwa huku kikipoteza wagombea 30 katika majimbo yote ya Zanzibar.

Alisema kuenguliwa huko kwa wagombea kunaweka historia mbaya katika uchaguzi, akibainisha kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 hadi 2010 haukuwa na dosari hiyo.

Kufuatia hali hiyo, Lissu alitoa tamko la chama kwamba wanataka wagombea wao nchi nzima warudishwe bila masharti yoyote vinginevyo watahamasisha wananchi wachukue hatua kufanya maandamano ya amani kushinikiza hilo.

"Tuchukue hatua, haki hailetwi kwenye kisahani cha fedha kama kifo cha Yohana mbatizaji, lazima idaiwe, ipiganiwe," Lissu alisema na kusisitiza kuwa hataanza mikutano ya kuomba kura bila wagombea wao kurudishwa.

Lissu pia aliomba jumuiya ya kimataifa iwaunge mkono kwenye hilo kwa kuwa ili uchaguzi ufanyike, lazima wawe na wagombea, akisisitiza "Jumuiya ya kimataifa iwachukulie hatua wahusika wote wa jambo hili."

Mgombea huyo pia alitumia nafasi hiyo kukiombea chama chake fedha kwa wananchi kwa ajili ya kampeni, akitangaza namba za benki watakazotumia kupokea fedha hizo.

**18 WAPETA NEC**

Wakati huo NEC imetangaza wagombea katika majimbo 18 ambao wamepita bila kupingwa na watatangazwa katika gazeti la serikali, ikisisitiza kuwa ni huru na inafanya kazi kwa kufuata sheria na katiba ya nchi.

Tume hiyo pia imewataka wananchi kuwa watulivu wakati ambao NEC inaendelea kushughulikia rufani zilizokatwa na wagombea mbalimbali.

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dodoma jana kuwa tume hiyo ni huru na haifanyi kazi kwa maelekezo na kuwaonya wanasiasa waache iliodai wanatisha wananchi. Aliyataja majimbo na wagombea wa CCM wamepita bila kupingwa kuwa pamoja na Elias Kwandikwa (Ushetu), Job Ndugai (Kongwa), Ahamed Shabiby (Gairo), Profesa Palamagamba Kabudi (Kilosa), Jonas Zeeland (Mvomero), Kalogereris Shabani (Mororgoro Kusini), Taletale Shabani (Morogoro Mashariki) na Isaac Kamwelwe (Katavi).

Wengine ni Geofrey Pinda (Kavuu), Philipo Mulugo (Songwe), Zedi Jumanne (Bukene), Dk. Hamis Kigwangalla (Nzega Vijijini), Kassim Majaliwa (Ruangwa), Nape Nnauye (Mtama), Vita Kawawa (Namtumbo), Jumanne Sagini (Butiama), Alexander Mnyeti (Misungwi) na Januari Makamba (Bumbuli).

Dk. Charles alisema majimbo hayo wagombea wake wameteuliwa kutokana na wengine kutokidhi vigezo na muda wa mapingamizi na rufani umepita.

"Tabia ya viongozi wa siasa kuwatishia watendaji wa tume ikome na ambao hawataridhika na uamuzi, wanayo fursa ya kukata rufani," alisema.

**Imeandikwa na Romana Mallya na Enock Charles DAR na Augusta Njoji, DODOMA**

# Kampuni yatozwa bilioni 12/- madai kuiba masafa

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Raha, imetozwa faini ya Sh. bilioni 11.89 kutokana na tuhuma za mbalimbali ikiwamo kutumia masafa ya mawasiliano ya redio bila leseni halali ya Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) tangu Machi 24, mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, James Kilaba, alitangaza adhabu hiyo jana jijini Dar es Salaam mbele ya waandishi wa habari, baada ya mamlaka hiyo kujiridhisha kuhusu makosa yaliyofanywa na kampuni hiyo.

Alisema wameitoza kampuni hiyo faini ya Sh. bilioni 11.85 kwa kutumia masafa ya mawasiliano ya redio katika wigo wa 1452-1482 MHZ.

Alisema kampuni hiyo pia imetozwa faini ya Sh. milioni 10 kwa kujenga miundombinu ya mfumo wa mawasiliano, kuendesha na kutoa huduma za mawasiliano katika Mkoa wa Mtwara bila leseni kutoka TCRA.

Kilaba alisema kampuni hiyo pia imetozwa faini ya Sh. milioni tano kwa kushindwa kujenga, kusimika, kuendeleza, kuendesha na kuwezesha upatikanaji wa miundombinu ya mawasiliano Mkoa wa Tanga kwa mujibu wa leseni yake.

Vilevile, alisema kampuni hiyo imetozwa faini ya Sh. milioni tano kwa kushindwa kuwasilisha kwa TCRA taarifa za ukaguzi wa hesabu zake ndani ya miezi sita na Sh. milioni tano nyingine kwa kushindwa kuwasilisha mpango mkakati wa mwaka wa kuendeleza rasilimali watu.

Kilaba alisema faini ya Sh. milioni 10 imetozwa kwa kampuni hiyo kwa kushindwa kutimiza masharti ya leseni na kushindwa kuomba upya leseni kwa muda uliopangwa.

"Raha Limited ikishindwa kutimiza masharti yote yaliyotolewa ndani ya siku 90, TCRA itachukua hatua zaidi za kiudhibiti dhidi yake," alionya Kilaba.

Mkurugenzi huyo alisema TCRA ilifikia uamuzi huo chini ya kifungu 48 (2) cha sheria ya kuanzishwa kwake Sura ya 172, iliyofanyiwa mapitio ya mwaka 2017, baada ya kuzingatia utetezi uliotolewa mbele yake na Kampuni ya Raha.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, SACP Henry Mwaibambe, akionyesha kwa waandishi wa habari, vipande 95 vya nyama ya pundamilia na vipande 109 vya nyumbu ambavyo ni nyara za serikali, walizozikamata katika Kijiji cha Mwasilimbi, Kata ya Ihusi, wilayani Bariadi jana. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Wanne zaidi wachukua fomu za urais Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDADI ya wagombea urais wa Zanzibar waliochukua fomu za kuomba uteuzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibra (ZEC) kuwania nafasi hiyo, imefikia tisa baada ya jana wagombea wanne kuchukua fomu hizo. Wagombea waliochukua fomu jana ni Ali Juma wa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Issa Muhammed Zonga wa chama cha Sauti ya Umma (SAU), Ameri Said Ameri wa chama cha Demokrasia Makini na Hamad Muhammed Ibrahim wa UPDP.

Akizungumza baada ya kuchukua fomu, mgombea wa CHAUMMA, Juma, alisema vipaumbele vyake akipata urais ni kutengeneza Zanzibar mpya yenye maendeleo kiuchumi.

Alisema atawafanya wazanzibari wenye upendo na kuondokana na chuki na uhasama wa kisiasa na uchaguzi wa mwaka huu utakuwa ni wa mabadiliko, Zanzibar ikitarajiwa kuondokana na siasa za mapambano ya chuki na kuwa na siasa za kushindana kwa fikra za kiuchumi na maendeleo.

Alisema atahakikisha upatikanaji wa katiba mpya kwa sababu ni kilio cha wazanzibar kwa miaka mingi, hivyo kulisimamia hilo kwa kushirikiana na Rais wa Tanzania.

"Nitahakikisha ninaimarisha upatikanaji wa elimu na wanafunzi wote wanapokuwa shuleni kupata chakula ili kuwa na ufahamu mzuri na kufaulu mitihani yao.

Mgombea wa SAU, Zonga, alisema atakapopata ridhaa ya kuwa rais, ataheshimu Mapinduzi ya Zanzibar, kudumisha amani na kuendeleza yote yaliofanywa na marais wa Zanzibar waliopita.

Alisema atahakikisha anaboresha sekta za kilimo, elimu, viwanda, ajira kwa vijana na kuwawezesha wazee na watu wenye ulemavu.

Mgombea wa chama cha Demokrasia Makini, Ameri, alisema endapo atapata ridhaa kuiongoza Zanzibar, atahakikisha anaiwezesha Zanzibar kiuchumi na kuifanya kuwa ya viwanda.

Aliahidi kuimarisha huduma za kijamii zikiwamo za afya na upatikanaji wa elimu bure ili nchi ipate maendeleo.

Hata hivyo, alisema atahakikisha anawalipa mshahara wananchi wote wasiokuwa na ajira kwa kila mwezi ili kujikimu kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Mgombea wa UPDP, Ibrahim, alisema akipata ridhaa ya kuwa Rais wa Zanzibar, atahakikisha anatoa adhabu kali kwa washtakiwa wote wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia ili vitendo hivyo vitokomezwe Zanzibar.

Alisema ataboresha huduma za kijamii ikiwamo, afya, elimu na miundombinu ya upatikanaji wa huduma za maji na salama.

Tume ya Uchaguzi Zanzibar itafunga milango ya uchukuaji na urejeshaji wa fomu za urais Septemba 9, mwaka huu. Kesho ni zamu ya chama cha NRA na Jumapili, DP na ACT-Wazalendo.

**MAALIM AWASILI ZANZIBAR**

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuwasili Zanzibar akitokea Dubai jana, Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, alisema yupo mzima wa afya na alikwenda huko kwa ajili ya mapumziko ya kujipanga kwa uchaguzi.

Aliwatoa wasiwasi wanachama, wafuasi na wapenzi wa chama cha ACT-Wazalendo kwamba yupo vizuri na afya yake ni njema, tofauti na ilivyodaiwa na baadhi ya watu kwamba alikwenda Dubai kwa ajili ya matibabu ya kibingwa.

"Nimewasili Zanzibar kutoka Dubai ambapo nilikwenda kwa ajili ya mapumziko mafupi kujiweka tayari kwa ajili ya zoezi la uchukuaji wa fomu na harakati za kampeni za uchaguzi mkuu wa Oktoba 28... msiwe na wasiwasi, ni mzima wa afya," alisema.

Mpaka jana, wagombea tisa waliokuwa wamechukua fomu ni Dk. Hussein Mwinyi (CCM), Said Soud (AAFP), Juma Ali Khatib (Ada Tadea), Hamad Rashid (ADC), Mfaume Khamis (NLD), Ali Juma (CHAUMMA), Issa Muhammed Zonga (SAU), Ameri Said Ameri (Demokrasia Makini) na Hamad Muhammed Ibrahim (UPDP).


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
24 – 08 - 2020

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumapili tarehe 30 – 08 – 2020** kampuni ya Mainline Carriers Ltd. itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam** kuelekea **Kiabakari Musoma,** gari hizo zenye namba za usajili:

**T 402 DFE / T 777 AQR**
**T 622 DFA / T 974 CPS**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.05** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.0** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port hadi Kiabakari Musoma** Kupitia Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu hadi Musoma gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Aliyempa JPM jogoo atoa siri

**Na Joseph Mwendapole**

MZEE Shaweji Kimbwembwe (72), aliyempa zawadi ya jogoo Rais John Magufuli mkoani Lindi, ameelezea sababu zilizomsukuma kufanya hivyo.

Akizungumza na kituo kimoja cha televisheni juzi, mzee huyo mkazi wa Kijiji cha Somanga, Kilwa mkoani Lindi, alisema aliona zawadi inayostahili kumpa Rais ni kuku kwa sababu yeye ni maskini na hakuwa na kitu kingine cha kumpa.

Kimbwembwe alimpa Rais Magufuli zawadi hiyo aliposimama kwenye kijiji cha Somanga alipokuwa akitokea mkoani Mtwara kwenye mazishi ya aliyekuwa Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa.

Mzee huyo alisema yeye anamiliki kuku tu na uwezo wake wa kumiliki fedha ni 10,000 hadi 30,000 hivyo aliona kuku ndiyo zawadi mwafaka kwa siku hiyo.

Alisema alisikia Rais Magufuli akitoa msamaha kwa wafungwa hali ambayo ilimgusa kwa kiwango kikubwa kutokana na wema huo.

Wakati huo, alisema alitamani sana kusafiri hadi jijini Dar es Salaam ili ampe mkono Rais Magufuli kutokana na wema huo lakini alishindwa kutokana na hali yake ya umaskini.

"Wakati ule anawasamehe wale wafungwa, machozi yalinilenga lenga. Nilisikitika tu umaskini huu ila nilitaka niende kumpa mkono wa pongezi Dar es Salaam na kumwambia asante," alisema.

Aliongeza kuwa tabia ya upendo, huruma na wema kwa kawaida mtoto huanza kuona kwa wazazi wake, hivyo anaamini kuwa Rais Magufuli aliiga upendo huo kutoka kwa mama na baba yake.

"Sasa inavyoonyesha ni kwamba mama na baba yake Magufuli kuna kitu kizuri walikifanya wakati wanamlea akiwa mdogo ndiyo maana nikaamua kutoa zawadi ya kuku kwa mama ambaye alilea kitu kizuri," alisema.

"Kuwa Rais si sababu ya kufanya wema mtu anaweza kuwa Rais na akawa na maamuzi (uamuzi) ya (wa) ovyo ovyo tu. Lakini huyu tuliye naye hayuko hivyo ndiyo sababu nikavutiwa naye," alisisitiza mzee Kimbwembwe.

Alimshukuru Rais Magufuli kwa kukubali kupokea zawadi ya kuku akisema kwa cheo alichonacho angeweza kudharau zawadi hiyo kwa kuona kuku atachafua gari lake.

"Angeweza kukataa na kuniambia asante sana nenda ukafuge mwenyewe lakini alikubali na akamchukua. Imenipa heshima sana hapa kijijini kwangu," alisema Mzee Kimbwembwe

Alimshukuru Rais Magufuli kwa zawadi ya Sh. 100,000 aliyompa kwa madai kuwa ilimsaidia kusherehekea siku ya Idd kwa shangwe kama watu wengine wenye fedha kijijini hapo.

Alisema ingawa yeye ni mtu wa kipato cha chini, kuna watu wengi wanamtegemea, hivyo kwa kuwa kesho yake ilikuwa sikukuu ya Idd, fedha hiyo ilimwezesha kula sikukuu vizuri.

"Kwa Kilwa ilivyo hapa Somanga ndiyo mjini sasa ile hela ilinifanya nikasherehekea sikukuu kama vile mtu aliyetoka mjini," alisema.



Magari yakiwa katika foleni kwenye barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, iliyosababishwa na upanuzi unaoendelea wa barabara hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mchungaji mbaroni madai ya upatu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MCHUNGAJI wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mbulu, Emmanuel Guse, anashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa madai ya kuendesha biashara ya mikopo umiza, maarufu kama upatu, bila kuwa na leseni.

Guse ambaye ni Mchungaji Kiongozi katika Usharika wa Ufana, alikamatwa jana na TAKUKURU baada ya mwananchi mmoja mkazi wa Bashnet, kushtaki kwa taasisi hiyo kuhusu mkopo wake wa Sh. 200,000 na kurejesha Sh. 400,000 lakini bado akawa anadaiwa Sh. 480,000.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Manyara, Holle Makungu, alithibitisha jana kukamatwa kwa mchungaji huyo ambaye pamoja na mambo mengine amekiri kufanya biashara hiyo bila kuwa na leseni.

"Baada ya malalamiko hayo, tulimtaka Mchungaji Guse aje kwa hiari yake katika ofisi zetu za mkoa, lakini akakaidi, hivyo tulilazimika kuwatuma makachero wetu kwenda kumkamata," alisema Makungu.

Alisema makachero walimkamata Mchungaji Guse na walimwuliza iwapo anafanya biashara ya kukopesha fedha lakini alikana na kudai kuwa hajawahi kufanya hivyo.

Mkuu huyo alisema makachero walilazimika kufanya upekuzi nyumbani na ofisini kwa mtuhumiwa hatimaye wakapata mikataba ya mikopo umiza 48.

"Baada ya kukusanya nyaraka katika upekuzi, makachero wetu walimchukua hadi ofisi zetu mjini Babati na kumhoji na alikiri kufanya biashara hiyo ya mikopo umiza bila leseni," alisema.

Pia alisema mtuhumiwa alipoulizwa kuhusu mlalamikaji, alikiri kuwa ni kweli alimkopesha Sh. 200,000 tu na kwamba amekwisha kurejesha Sh. 400,000 tu lakini bado anadai tena sh. 480,000.

Aliongeza kuwa mchungaji huyo anaendelea kushikiliwa na TAKUKURU Manyara wakati wakiendelea na uchunguzi wa mikataba umiza 48 iliyokutwa nyumbani kwake wakati wa upekuzi.

## Mgombea urais aliyekatwa NEC sasa kikaangoni

**Na Thobias Mwanakatwe**

CHAMA Cha Kijamii (CCK), kimepanga kuitisha kikao cha kumweka kitimoto aliyekuwa mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia chama hicho, David Mwaijojele, kutokana na kuenguliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwania nafasi hiyo.

Mwaijojele ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCK, alienguliwa kuwania urais baada ya mgombea mwenza wake kutohudhuria urejeshaji wa fomu katika ofisi za tume jijini Dodoma.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Renatus Muabhi, akizungumza na Nipashe jana, alidai Mwaijojele alikuwa na uhusiano mbovu na viongozi wenzake na ndicho kiini cha kutopewa ushirikiano tangu mwanzo wa mchakato.

"Tutaitisha kikao ambacho kitahoji mwenendo mzima ulivyofanyika mpaka kukifikisha chama kwenye hatua hii, tunafahamu mchakato huu ulikuwa wa kifamilia, haukuwa na baraka za kichama," alidai.

Akijibu tuhuma hizo, Mwaijojele alisema kuenguliwa kwake na NEC hakukutokana na kususwa na viongozi wenzake wa chama hicho.

"Wewe unafahamu masharti ya uchaguzi hasa kwa nafasi ya rais, hauwezi ukaendesha uchaguzi kifamilia, maana unakuwa na fomu 14 mikoa ya Tanzania Bara na miwili ya Zanzibar. Sasa ni familia gani inaweza ikaenda huku bara na visiwani?" alihoji.

Mwaijojele alisema mkutano mkuu wa chama ambao pia ulihudhuriwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, ndiyo uliompitisha kuwania urais kwa kura zote.

"Kwanza, Muabhi ni mwanachama wa kawaida, siyo Katibu Mkuu wa chama, alikuwa kiongozi zamani, lakini akaondolewa kwenye nafasi hiyo kwa taratibu za chama," alisema.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), James Kilaba (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ukiukwaji wa sheria, kanuni, taratibu na masharti ya leseni, uliofanywa na kampuni ya Raha Ltd.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wadaiwa kufanya vikao usiku kuhujumu CCM

**Na Jumbe Ismailly,** HANANG

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Hanang, mkoani Manyara, kimewatahadharisha baadhi ya viongozi wa chama wanaofanya vikao usiku vya kukihujumu chama hicho.

Kimeonya na kusema hakitasita kuwachukulia hatua za kisheria kwa kufanya vikao vyao bila kuwa na vibali.

Mkuu wa Wilaya ya Hanang, ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya wilaya hiyo, Ghaib Lingo, alitoa tahadhari hiyo kwenye mkutano wa hadhara wa kuwatambulisha wagombea wateule wa ubunge na udiwani uliofanyika kwenye viwanja vya michezo vya Kijiji cha Endasak.

Alisisitiza kuwa kamati ya siasa katika uchunguzi uliofanywa na vyombo vya dola, umebaini kwamba kuna baadhi ya viongozi wa kata tano za wilaya ya Hanang wanaojihusisha na vikao vya usiku huku wakitambua kuwa kufanya hivyo ni kuvunja sheria za nchi.

Lingo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, alisema baadhi ya viongozi hao baada ya majina ya wagombea wao kutoteuliwa na vikao vya juu, wameanza kukaa na wanachama na wananchi kwenye maeneo yao na kuwashawishi kuinyima kura CCM na badala yake wapigie kambi ya upinzani.

"Nina kata tano ambazo viongozi wa chama wanafanya kazi hizo usiku, nilikuwa nafikiri siku nikiamka vibaya niwashike niwaweke ndani kwa sababu kufanya mikutano usiku bila kibali cha polisi ni kosa. Mimi nitashindwa kukutungia kesi wewe kwani hata leo tumepata kibali cha polisi ndiyo tunakutana hapa," alisema.

Aliweka bayana kuwa baada ya wagombea wateule wa ubunge na udiwani kutambulishwa kwa wanachama na wananchi kwa ujumla, aliwaomba kuwachagua viongozi walioteuliwa na chama hicho ili waweze kuwaletea maendeleo endelevu.

Mkuu wa wilaya huyo alisisitiza kwamba ili wananchi wa Hanang wamlaumu mwakilishi wao wa ubunge kwamba ameshindwa kutekeleza ahadi za maendeleo, hawana budi kuhakikisha wanawachagua wagombea wateule wote walio pendekezwa na chama hicho.

Alisema ifikapo Oktoba 28, mwaka huu, wanachama wa chama hicho na wananchi wa Hanang kwa ujumla wahakikishe kura za kishindo zinakwenda kwa mgombea wa urais, wabunge na madiwani wa CCM kukamilisha mafiga matatu.

Akiwatambulisha wagombea wateule wa ubunge na udiwani wapatao 33, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Hanang, Mathew Dalema, alisema baada ya wagombea hao kuteuliwa na vikao vya juu vyenye mamlaka ya kufanya hivyo, kazi iliyobakia ni kuwanadi wapigakura ili kushinda kwa kishindo.

# Kortini madai ya kuhujumu miundombinu ya TANESCO

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Anuary Hamdani (29) na fundi umeme Joseph Oswald (31), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakikabiliwa na shitaka la kuhujumu miundombinu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Luboroga.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Maternus Marandu, alidai kuwa washtakiwa walitenda kosa hilo Agosti 7, mwaka huu, eneo la Magomeni Mikumi, jijini Dar es Salaam.

Ilidaiwa kwamba kwa nia ovu, washtakiwa hao kwa pamoja waliingilia miundombinu ya shirika hilo kwa kuondoa mita ya umeme ya TANESCO kutoka nyumba ya Ahmed Hamdani iliyokuwa na deni.

Ilidaiwa kwamba mita hiyo ilikuwa na deni la Sh. 3,521,587.70 na kuwekwa mita nyingine mpya kwa lengo la kukwepa deni hilo.

Baada ya kusomewa shitaka hilo, washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu lolote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Upelelezi wa kesi hiyo unaendelea, mshitakiwa Amdani aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya dhamana na Oswadi alishindwa masharti na kupelekwa rumande.

Miongoni mwa masharti hayo ni kila mshitakiwa kuwa na wadhamini wawili watakaosaini bondi ya Sh. 500, 000.

Kesi imeahirishwa hadi Septemba 10, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.

# Kijana aomba msaada tiba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKAZI wa Kizota jijini Dodoma Mathayo Kudenya (25) anaomba msaada wa Sh. 800,000 ili afanyiwe upasuaji wa kutoa maji katika korodani zake, tatizo linalomsumbua kwa zaidi ya miaka mitano sasa.

Akizungumza na Nipashe nyumbani kwao, Kudenya alisema tatizo hilo lilianza mwaka 2015 na amezunguka katika maeneo mbalimbali bila kupata tiba.

Kudenya alisema tatizo hilo lilianza baada ya kutoka jando mwaka 2015, ambapo alianza kuhisi muwasho na baadaye vikatokea vidonda katika nyonga zake ambavyo vilikuwa vikitoa maji.

"Nilikua nahisi muwasho kwenye korodani zangu muda mfupi vikatokea vidonda katika maeneo ya nyonga vilikuwa vinatoa maji, lakini baada ya kukauka ndipo korodani zikaanza kuvimba na kuja maji hadi kufikia hali hii,"alisema Kudenya

Alisema alizunguka katika maeneo mbalimbali hadi kwa waganga wa kienyeji katika Mkoa wa Tanga na kutumia dawa bila mafanikio.

"Nilikwenda kwa waganga Tanga na maeneo ya Chamwino mkoani Dodoma, ambapo wataalamu walinipa dawa bila mafanikio na kunishauri pia niende katika hospitali kubwa ili kubaini nini kinanisumbua," alisema Kudenya.

Kadhalika, alisema kutokana kuendelea kupata maumivu, Aprili, mwaka huu alikwenda katika Hospitali ya Benjamini Mkapa jijini Dodoma na kufanyiwa vipimo.

"Baada ya kufanyiwa uchunguzi madaktali waliniambia kuwa nina tatatizo la kujaa maji kwenye korodani zangu ninatakiwa kutoa Sh. 800,000 na chupa tatu za damu ili kufanyiwa upasujai," alisema huku akidai kuwa kutokana na hali duni ya maisha aliyo nayo, hataweza kumudu gharama hizo.

Bibi wa kijana huyo, Janeth Mafupi, alisema hivi sasa hali ni mbaya na anawaomba wasamalia wema kumsaidia mjukuu wake ili afanyiwe upasuaji na kurudi katika shughuli zake za kujitafutia kipato kama awali.

"Kama kuna mtu ataguswa kutusaidia ili kupata matibabu ya kijana wetu ili arudi katika hali yake ya awali tunaomba awasiline na familia kupitia namba ya simu 0713 533337," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Namungo soka la kiungwana litawale kesho

**KIPENGA** cha msimu mpya wa Ligi Kuu Bara, kinatarajiwa kupulizwa kesho kwa mabingwa wa Ligi Kuu Bara na Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF) maarufu FA Cup, Simba kushuka dimbani dhidi ya Namungo FC kuwania Ngao ya Jamii katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kawaida pazia hilo hufunguliwa kwa mechi ya Ngao ya Jamii ambayo humkutanisha bingwa wa Ligi Kuu dhidi ya mshindi wa Kombe la FA, lakini kutokana na Simba kubeba mataji yote mawili msimu uliomalizika, Namungo imepata nafasi hiyo kutokana na kucheza fainali ya FA Cup.

Kupigwa kwa mechi hiyo ni ishara ya kufunguliwa kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2020/21, unaotarajiwa kuanza rasmi Septemba 6, mwaka huu ukishirikisha timu 18 badala ya 20 kama ilivyokuwa msimu uliopita.

Makocha wote wawili wa timu hizo, Kocha wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck na yule wa Namungo, Mnyarwanda Thierry Hitimana, kila mmoja ameeleza nia yake ya kutwaa ubingwa huo, lakini wakikiri haitakuwa mechi rahisi hata kidogo.

Hii itakuwa mechi ya nne timu hizo kukutana, ambapo Simba imeshinda mechi mbili na moja zikitoka sare, hivyo Namungo itakuwa na nafasi ya kujiuliza zaidi ni wapi inakwama kupata matokeo inapokutana na mabingwa hao mara tatu mfululizo wa Ligi Kuu Bara.

Tunatambua itakuwa ni mechi ya kuvutia hasa tukizingatia ni mchezo unaozikutanisha timu mbili zenye tiketi ya kuipeperusha bendera ya Tanzania kimataifa; Simba ikiwa na jukumu la kuhakikisha inaipeperusha vema kwenye Ligi ya Mabingwa wakati Namungo ikitegemewa kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Aidha, timu hizo zinashuka dimbani kila moja ikiwa imeonyesha kiwango cha kuvutia kwenye mechi za kirafiki ilizocheza, ambapo, Simba mbali ya kushinda dhidi ya KMC 3-1 na Transit Camp 5-0, mechi ambayo mashabiki walishuhudia viwango vya wachezaji wa mabingwa hao ni dhidi ya Vital'O ya Burundi kwenye tamasha la Simba Day wakishinda 6-0. Lakini pia, Namungo ilionyesha soka la kuvutia wakati ikikubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Azam FC kwenye tamasha la Azam Festival.

Hivyo, mashabiki wa timu hizo na wadau wa soka nchini kwa ujumla, wanatarajia kushuhudia kandanda safi na la kuvutia, lakini pia wakitumia mchezo huo kutathimini vikosi vyao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano ya kimataifa kwa wawakilishi hao wa Tanzania Bara.


Nipashe kama ilivyo kwa wadau wengine wa soka, pia tunatarajia kuona soka safi na la kuvutia mwanzo mwisho ambalo si tu litatoa tathimini ya vikosi vyao kuelekea michuano ya kimataifa na Ligi Kuu, bali utatumika kujua upinzani utakavyokuwa kwa timu 18 zitakazoshiriki Ligi Kuu Bara msimu wa 2020/21.

Tunatarajia pia kuona waamuzi wakitenda haki kwa kufuata sheria 17 za soka na kutokuwapo kwa timu moja kubebwa katika mchezo huo ambao utakuwa mara ya kwanza kuchezwa katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Na kwa upande wa wachezaji, tunatamani kuona wakionyesha kandanda safi na kutocheza kwa kukamiana na rafu zisizo za msingi kwani kwa kufanya hivyo, kutawasababishia majeraha yasiyo ya lazima kuelekea msimu mpya.

Ingawa upinzani hauwezi kuzuilika huku kila timu ikihitaji kufungua msimu kwa kutwaa taji la kwanza, wachezaji wanapaswa kutanguliza mbele utu wa kila moja kwa kucheza soka la kiungwana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba, Yanga, yetu macho

**'TAMBO'** ni mtindo wa usemaji wa kufumba ili mtu mwingine afumbue. Pia gimba yaani uwiano wa unene na urefu wa umbo la mtu; jirimu. Aidha, mtu au kitu kinavyoonekana kama kilivyo. Kitanzi, yaani kitu au jambo lililotengenezwa au kufanywa kwa ustadi wa hali ya juu. Hili ndilo ninalolizungumzia leo.

Neno 'tamba' nalo lina maana zaidi ya moja. Hata hivyo ninalolijadili ni kutembea kila mahali kwa kujifaragua, yaani kitendo cha mtu kufanya jambo kama anavyopenda bila kuingiliwa; jigamba, jifanya kujua sana. Kitendo cha mtu kukosa mwingine anayelingana naye kwa uwezo au ujuzi. Hivi ndivyo zilivyo Simba na Yanga kila msimu unapoanza.

Wahenga walituachia methali zenye mafunzo mengi kwetu. Kati ya methali hizo ni ile isemayo: "Maneno ni daraja, hayazuii maji kuteremka." Maana yake daraja haliwezi kuyazuia maji ya mto yasiteremke; maneno nayo hayawezi kumzuia mtu kufanya jambo aliloazimia.

Methali hii hutumiwa kumnasihi mtu aliyeazimia kufanya jambo fulani asikate tamaa au asivunjwe na maneno ya watu ambayo hayamdhuru kwa namna yoyote. Huweza pia kutumiwa na mtu aliyeazimia kufanya jambo fulani kujitetea dhidi ya maneno ya binadamu.

Yanga na Simba ndizo timu kongwe zaidi nchini zinazofahamika zaidi Tanzania, Afrika Mashariki na Afrika kwa jumla. Timu hizo zimeiwakilisha Tanzania mara nyingi zaidi kwenye michezo ya kimataifa ingawa hakuna hata moja iliyoshinda na kutwaa ngao wala kombe.

Young Africans ilianzishwa mwaka 1935. Nadhani neno 'Young' liliwapa shida jinsi ya kulitamka, ikaitwa kwa ufupi 'Yanga.' Mwaka uliofuatia, yaani 1936 ikaanzishwa klabu iliyoitwa Sunderland kwa kuiga jina la moja ya timu za Uingereza. Kama ilivyokuwa kwa wenzao, jina 'Sunderland' nalo likarahisishwa na kuitwa 'Sanda' ingawa halina maana nzuri kwa timu kwani maana ya neno hilo ni kitambaa cheupe anachovikwa maiti wa kwa utaratibu maalumu na kuzikwa nacho. Pia ni pesa wanayopewa wafiwa kusaidia kulipa gharama za mazishi; ubani.

Hata hivyo, klabu hiyo ilibadili jina na kuitwa Simba (mnyama anayeitwa mfalme wa mwitu) siku ilipofunguliwa jengo lao jipya pale Msimbazi na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abeid Aman Karume (Mungu amrehemu). Je, sasa timu ya Simba imekuwa 'mfalme' wa timu za kandanda nchini kwa kutwaa ngao na vikombe mbalimbali nchini kwa msimu mmoja?

'Bidii' ni jitihada katika kutekeleza jambo lolote; juhudi, idili. Ndivyo ilivyofanya Simba kwenye Ligi Kuu ya msimu uliopita. Timu hiyo imethibitisha kuwa "Penye nia pana njia" kwani mtu akiwa na dhamira ya kufanya jambo fulani hawezi kuikosa njia. Twakumbushwa kwamba tuwapo na nia ya kufanya jambo fulani lazima tutafanikiwa.

Kijana MO Dewji ndiye chanzo na kiini cha Simba kuwa tishio kwa timu zingine nchini na twaomba mafanikio hayo yawe hivyo hata itakapopambana na timu za nje ya Tanzania. Naomba kwa dhati nikiweka kando mvutano uliopo baina ya Yanga na wapinzani waou wa jadi, Simba. Kijana MO Dewji amekuwa msaada mkubwa kwa Simba akigawa fedha kama peremende ili kufanikisha kila aliloambiwa au aliloona linafaa. Yote hayo yathibitisha mapenzi yake kwa Simba, mbali ya kuwa mwekezaji mwenye asilimia 49 ya hisa.

Sasa macho yote ya viongozi, wanachama na mashabiki wa Yanga yanakodoa kwa Kampuni ya GSM ambayo sasa ndio inayoifadhili Yanga kwa kila kitu. Ni muhimu sasa mkataba wa Yanga na klabu ya Hispania ufanyiwe kazi kwa umakini zaidi. Nasema hivyo kwani kama utatumika vizuri, hapana shaka Yanga itajifunza mengi yatakayoiletea maendeleo. Yanga yaweza kupata wataalamu watakaosaidia kuanzisha shule za wachezaji wadogo na wakubwa kupata nafasi kwenye timu za ughaibuni kirahisi zaidi.

Muhimu ni viongozi wa klabu kuwa makini na waaminifu katika matumizi ya hela, vinginevyo wadhamini watajitoa. Ule usemi wa 'kupiga pesa' usiwapo na kama wapo wanaokusudia kujinufaisha, wajitoe kabla ya kutimuliwa kwa fedheha.

Pia itayarishwe katiba mpya itakayokubaliwa na wanachama na serikali sawia kwa manufaa ya pande zote, yaani wafadhili (GSM) na wafadhiliwa (Yanga).

Jambo lingine la kuzingatiwa ni kutokuwa na usiri wa mambo yanayokusudiwa kufanywa na klabu. Msemaji wa klabu ni mtu anayetangaza mambo ya klabu inapolazimika.

Hata viongozi wakuu wanapotaka kutangaza jambo fulani, hupewa msemaji wa klabu ili autangazie umma. Mambo yanayokusudiwa kufanywa na klabu, kama vile usajili wa wachezaji wapya n.k. ni kazi ya msemaji.




Mkuu Msaidizi wa Shule ya Sekondari Baobab iliyopo Mapinga wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, Alphonce Francis (kushoto), akiwaasa wanafunzi wa shule hiyo jana, kusoma kwa bidii kama wenzao 423 wa kidato cha sita ambao wote wamefanikiwa kujiunga vyuo vikuuu mbalimbali ndani na nje ya nchi **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Watano wafariki ajali ya basi, gari dogo

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WATU watano wamefariki dunia papo hapo katika ajali iliyohusisha gari ndogo lililogongana na basi la kampuni ya NBS lenye namba za usajili T,571 BPZ katika kijiji cha Nyasamba, Kishapu mkoani Shinyanga barabara ya Shinyanga - Mwanza.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Debora Magiligimba, alisema ajali hiyo imetokea juzi, majira ya saa 9:00 mchana.

Magiligimba alisema chanzo cha ajali hiyo ni gari dogo aina ya Toyota Secceed kukosa mwelekeo na kugonga basi dogo aina ya TATA mali ya Kampuni ya NBS lililokuwa likitoka jijini Mwanza kwenda Tabora. "Gari lenye namba za usajili T571 BPZ aina ya TATA Mini Bus ikiendeshwa na Kazimili Maganga, likitokea Mwanza kwenda Tabora, lilipofika eneo la Nyasamba liligongana na gari lingine dogo lililokuwa likitokea Dar es Salaam likiendeshwa na Ramadhan Siraji na kusababisha vifo vya watu watano", alisema Magiligimba.

"Chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa madereva wa magari yote mawili na uzembe wa dereva wa gari dogo ambaye alihama upande wa kushoto na kuendeshea kulia zaidi na kwenda kugongana na basi hilo na kusababisha vifo vya watu watano," aliongeza.

Kamanda magiligimba aliwataja waliofariki dunia katika ajali hiyo kuwa ni Ramadhan Siraji, Godfrey Gaspar, Anthony Pastory, Mallya Wambura na Abdul Juma na kwamba miili ya marehemu imehifadhiwa katika chumba cha maiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga.

Aidha alisema dereva wa kwenye gari dogo alifariki dunia huku wakimshikilia dereva wa basi la NBS, Kazimili Maganga, kwa hatua zaidi za kisheria.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo, baada ya ajali kutokea, gari dogo liliburuzwa na basi na kwamba dereva wa gari dogo alikuwa anaendesha kwa mwendokasi na tairi likapasuka ndipo ikatokea ajali

# Mgombea wa ubunge CHADEMA aenguliwa kwa kughushi saini

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MSIMAMIZI wa Uchaguzi wa Jimbo la Msalala, Simon Berege, ametengua uteuzi wa nafasi ya ubunge katika jimbo hilo kupitia chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kitundu Jedidiah David.

Hatua hiyo imetokana na msimamizi huyo kuridhika na pingamizi lililowekwa na mgombea wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Iddi Kassim Iddi, Agosti 26,mwaka huu.

Berege alisema mgombea huyo wa CHADEMA aliwekewa pingamizi kwamba David hakudhaminiwa na chama cha siasa kugombea nafasi hiyo.

Alisema pingamizi hilo lilikubaliwa kutokana na kuthibitika kugushiwa kwa saini ya Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Shinyanga, Zakaria Obad na kufanya uamuzi huo kwa mujibu wa kifungu cha 40(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343.

Kutokana na kuenguliwa kwa mgombea huyo wa CHADEMA, wagombea ubunge katika jimbo hilo sasa wamebaki watatu. Wagombea waliobaki ni Iddi (CCM), Machaga Machimbi (NCCR Mageuzi) na Jilala Seni (ACT Wazalendo)

# Ufaransa, Norway zapongezwa ufadhili miradi ya umeme vijijini

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Tanzania imezishukuru Ufaransa na Norway kwa mchango zilioutoa na kuendelea kutoa katika kuwezesha utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alitoa shukrani hizo juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa kikao baina yake na Balozi wa Ufaransa nchini, Frederic Clavier pamoja na Bjorn Midthun, ambaye ni Ofisa Mwandamizi kutoka Ubalozi wa Norway nchini Tanzania.

"Mmefanya kazi nzuri sana katika kutuwezesha kutekeleza miradi ya umeme vijijini. Ushirikiano wenu umetuwezesha kufikia hatua hii tuliyopo leo. Kwa niaba ya serikali, ninawashukuru sana," alisema Waziri. Dk. Kalemani alisema kutokana na ushirikiano na mchango wa nchi hizo, hadi sasa vijiji 9,512 ambavyo ni zaidi ya asilimia 85 ya vijiji vyote 12,268 vilivyoko nchini, vimeshafikiwa na umeme.

Alieleza ujumbe huo kuwa vitongoji takribani 25,000 vimeshafikishiwa umeme kati ya 64,339 vilivyoko nchini, hivyo akaziomba nchi hizo kuendelea kutoa mchango wao katika kuwezesha kutekeleza kazi iliyobaki.

Waziri alisema umeme ni injini ya uchumi na kwamba pasipo umeme wa uhakika, haiwezekani kwa nchi yoyote kuwa na maendeleo ya kiuchumi.

Aliongeza kuwa jitihada za makusudi zinazoendelea kufanywa na serikali hususani katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme, pamoja na mambo mengine, ndizo zimeiwezesha Tanzania, kuingia katika uchumi wa kati.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Balozi Clavier na Midthun, walimhakikishia Waziri Kalemani kuwa serikali za nchi zao zitaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuwezesha miradi mbalimbali ya umeme.

Pia viongozi hao walisisitiza umuhimu wa kuzingatia viwango vya ubora katika kutekeleza miradi husika na Waziri Kalemani aliwahakikishia kuwa ubora na uaminifu ni masuala yanayopewa umuhimu wa hali ya juu.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Styden Rwebangira; Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga na baadhi ya maofisa waandamizi kutoka REA, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Balozi za Norway na Ufaransa nchini.

# RC ataka viongozi goigoi kuachia ngazi

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amesema viongozi wa kata na tarafa zitakazobainika kuendelea kuwa na migogoro ya wakulima na wafugaji, wajiandae kuachia ngazi katika nafasi zao.

Ndikilo aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wakazi wa kata za Mkongo na Ikwiriri wilayani hapa katika ziara yake ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Akiwa katika kata ya Mkongo, wananchi walilalamikia kuhusiana na uwapo wa wafugaji ambao wamekuwa wakilisha mifugo yao katika mashamba ya wakulima hali inayohatarisha uwepo wa njaa kwa wananchi.

Seif Lwambo, mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Kilimani, Kata ya Mkongo, alimweleza Mkuu huyo wa mkoa kuwa, pamoja na mazao yao kusombwa na mafuriko, wafugaji nao wamekuwa chanzo cha kukosekana chakula.

"Mafuriko yalipita tukapanda mazao yetu na hawa wafugaji wakaleta mifugo yao wakalisha shambani kwetu. Hatuna chakula wao ndio wanatusababishia njaa. Mnaweza mkahangaika kujenga kituo hiki cha afya lakini kama suala la wafugaji halitadhibitiwa, hakuna mtu atafika kutibiwa hapa watu watakufa njaa," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alimwomba Mkuu wa Mkoa kuhakikisha wafugaji ambao wamekuwa kero kwao, wadhibitiwe ili wakulima walime maeneo makubwa ya kutosha kwa ajili ya kuepuka baa la njaa.

Ndikilo alitoa mwezi mmoja kwa maofisa tarafa wa Mkongo na Ikwiriri pamoja na watendaji wa kata na vijiji kujitathmini kabla hawajafukuzwa kazi kwa kushindwa kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji. Pia aliagiza kutoa ushirikiano kukamatwa wafugaji wanaolalamikiwa.

Mkuu wa Mkoa pia alitoa wiki moja kwa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Rufiji, Wilbert Siwa, kuhakikisha anamtia mbaroni mfugaji anayedaiwa kumbaka bibi na kumsababishia majeraha.

Katika tukio hilo, inadaiwa mfugaji ambaye ni jamii ya kisukuma, alimwingilia bibi huyo bila makubaliano ikiwa siku chache baada ya mazao yake kuliwa na mifugo.

Ndikilo alitoa fedha za nauli kwa ajili ya bibi huyo kufika kituo cha afya kupata matibabu baada ya kukwama kwa kukosa nauli. Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Luteni Kanali Patrick Sawala, alisema atasimamia maagizo yaliyotolewa ikiwa ni pamoja na kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji inayotokea mara kwa mara ili wananchi wafanye shughuli zingine za maendeleo.



Mfanyabiashara akiondoa mfuko wa uchafu uliotupwa na watu wasiojulikana kwenye meza zilizotelekezwa na wafanyabiashara wa mbogamboga na matunda katika soko la Sabasaba, jijini Dodoma jana, ambao walitakiwa kuhamia sokoni hapo kwa muda mrefu sasa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wazee kunufaika na matibabu bure

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHIRIKA la Tunajali lenye zahanati iliyopo Kwa Mathasi, kata ya Mkuza, Halmashauri ya Mji wa Kibaha linatarajia kutoa huduma ya vipimo na matibabu bure kwa wazee 600.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Nicas Mawazo, aliliambia gazeti hili jana kuwa huduma hiyo itafanyika Septemba 5, mwaka huu kuanzia saa 11: 00 alfajiri hadi jioni na wazee kutoka katika maeneo ya mji wa Kibaha ndio walengwa.

Mawazo alisema katika utoaji huduma hiyo, madaktari bingwa wa macho, moyo na magonjwa yasiyoambukiza, watawapatia huduma wazee wenye umri kuanzia miaka 50 watakaofika katika zahanati hiyo. Alisema huduma hiyo ya vipimo na matibabu, inafanyika siku chache baada ya ile iliyotangulia mwanzoni mwa mwezi huu. Zaidi ya wazee 300 walipata huduma ya vipimo, dawa na upasuaji kutoka shirika hilo.

Mkurugenzi huyo alisema huduma hiyo inatolewa kwa ushirikiano wa shirika hilo na benki ya CRDB.

"Tumeshafanya zoezi (huduma) kama hili kwa kundi la wazee, watoto na wanawake na sasa tumeona turudie tena kwa upande wa wazee kwani awamu iliyopita wengi walibainika kuwa na magonjwa yasiyoambukiza. Tutawapima bure na matibabu watapata bure," alisema.

Ninachowaomba mashirika mengine kusaidia jamii kwa kile wanachokipata kadri ya uwezo wao. Sisi huduma zetu zitakuwa endelevu tunacholenga ni kusaidia makundi haya kwa kusogeza huduma karibu na maeneo yao," alisema

# Baobab yataja siri kupeleka mamia vyuo vikuu

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Sekondari Baobab iliyoko Mapinga, Bagamoyo mkoani Pwani, imefaulisha wanafunzi 423 waliofanya mtihani wa kidato cha sita kujiunga na vyuo vikuu na vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Kutokana na kufaulisha huko, uongozi wa shule umetaja sababu za kufanya hivyo kuwa ni mazingira rafiki na ushirikiano kati ya uongozi, walimu, wanafunzi na wazazi.

Akizungumza na gazeti hili jana shuleni hapo, Mkuu wa Shule hiyo, Venance Hongoa, alisema wanafunzi 43 wamepata daraja la kwanza na 208 daraja la pili wakati wanafunzi 172 wamepata daraja la tatu.

Alisema matokeo hayo ni mazuri sana kwao kwa sababu wamekuwa wakichukua wanafunzi wenye ufaulu wa kawaida sana na wengi waliowachukua ni wale waliofanya usaili na wakakosa nafasi shule zingine.

Kwa mujibu wa Hongoa, mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo, Sheila Ntisi, amekuwa mwanafunzi wa nne kitaifa kwenye matokeo hayo na kwamba huo ni mwendelezo wa kufanya vizuri kitaaluma baada ya mwaka jana kutoa mwanafunzi bora kitaifa kwenye somo la biashara, Noreen Lyimo.

"Sisi tunachukua wanafunzi wenye ufaulu wa wastani wanaofundishika na kuwaandaa na sasa wamefaulu vizuri sana, tunajivunia kwa hilo kwani kuna wenzetu huchukua wanafunzi wenye vipaji sisi huwa hatuangalii hilo," alisema Hongoa.

Alisema wanafunzi saba waliingia kidato cha tano wakiwa na daraja la tatu lakini wamemaliza kwa kupata daraja la kwanza, wakati wanafunzi 47 waliingia wakiwa na daraja la tatu na kumaliza wakiwa na daraja la pili na wengine 15 waliingia wakiwa na daraja la pili na kumaliza wakiwa na daraja la kwanza.

"Kwa kulinganisha na walivyoingia, matokeo haya ni mafanikio makubwa sana kwetu na kazi kubwa sana imefanyika.

Tunashukuru juhudi za walimu na ushirikiano wa wazazi, uongozi wa shule na wanafunzi wenyewe," alisema.

Alisema hata kwenye matokeo ya kidato cha pili na cha nne, wamekuwa wakifaulisha wanafunzi wengi kwa daraja la kwanza na la pili kutokana na jitihada kubwa inayofanywa na walimu na uongozi wa shule hiyo.

"Tunashukuru kipekee uongozi wa shule na walimu kwa namna wanavyotupa ushirikiano mkubwa kuhakikisha shule yetu inaendelea kuwa juu mwaka hadi mwaka, tunawaomba waendelee kutupa ushirikiano kama huo ili Baobab izidi kuwa juu," alisema.

Alitaja siri ya mafanikio hayo kuwa ni mazingira bora ya kufundishia yaliyowekwa na uongozi wa shule hiyo kwa walimu na wanafunzi ikiwamo maabara na maktaba za kisasa za shule hiyo.

"Huduma bora za chakula, malazi, na zahanati iliyoko ndani ya shule ni miongoni mwa vichocheo ya mafanikio yetu, tumehakikisha afya imara za wanafunzi maana hawahitaji kwenda nje ya shule kwa matibabu wanatibiwa hapahapa," alisema





# Mauaji vurugu za kisiasa yamwibua Askofu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Masasi, Dk. James Almasi, amelaani tukio la mtu mmoja kupoteza maisha Tunduma, mkoani Songwe kutokana na vurugu za kisiasa na kuwataka viongozi wa dini kukemea vitendo hivyo.

Dk. Almasi alisema jana kuwa kitendo hicho ni kukiuka maagizo ya Mungu kuhusu amani ambayo imeanza kuchafuliwa na vyama vya siasa.

Alisema pamoja na viongozi wa dini na serikali kuiombea amani hiyo itawale kwenye mchakato wote wa uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu, baadhi ya watu wanaziharibu jitihada hizo.

Dk. Almasi alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu, Dayosisi ya Central Tanganyika (DCT) mjini hapa.

Alisema katika kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu ambao vyama vingi vya siasa vimejitokeza, ni muhimu Watanzania kuwa waangalifu kwa kuwachagua wagombea ili wasije kufanya makosa yaliyoanza kujitokeza ya mauaji ambayo yameanza kutia doa ndani ya taifa. Mapema wiki hii, mkoani Songwe, mtu mmoja alifariki dunia na watatu kujeruhiwa kutokana na vurugu za kisiasa zilizotokea zinazodaiwa kusababishwa na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Kiongozi huyo wa kanisa alisema kutokana na tukio hilo lililotokea alitakiwa kulaaniwa na kukemewa na vyombo husika ikiwamo viongozi wa dini ambao wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha amani iliyopo haipotei.

"Tunatakiwa kulaani vitendo hivi na kuhakikisha kuwa amani iliyopo nchini haiharibiwi na chama chochote kile cha kisiasa hasa kwa kipindi hiki tulicho nacho cha kuelekea uchaguzi mkuu wa 2020," alisema Askofu.

Katika hatua nyingine, askofu huyo aliwaomba Watanzania katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu, kutowachagua viongozi wenye uroho wa madaraka, wababe na wanaotanguliza maslahi yao badala ya wananchi.

Pia aliwaomba Watanzania kwenye uchaguzi mwaka huu pia kuviepuka vyama vya siasa ambavyo vinahatarisha uvunjifu wa amani ya nchi na nje ya mipaka.

Alisema kuna baadhi ya watu waliojitokeza ndani ya vyama vya siasa ambao wapo kwa dhana ya kutaka nafasi hizo kwa ubabe, uroho na utashi kwa ajili ya maslahi yao binafsi

"Mungu ndiye anayechagua wateule wake na sisi wanadamu tunatumiwa tu, hivyo hakuna sababu ya kungangania kwenye nafasi hiyo huku ukifahamu mwenye Mamlaka ni yeye mwenyewe" alisema.

Aidha, aliwaonya viongozi wanaogombea kutotafuta nafasi hizo kwa njia za rushwa kwa kuwa ni dhambi, wanachotakiwa kumuomba Mungu kwa uaminifu na sivyo vinginevyo.

"Kiongozi mzuri ni yule anayepatikana kutokana na vigezo vya Mungu, siyo kwa njia za waganga wa kienyeji vitendo vya kutoa rushwa au kwa kutishia watu kwa ubabe," alisisitiza.



Mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Elshadai, Betha Maganga (kushoto) na mwenzake wa darasa la saba, Cavin Willson, wakielezea jinsi walivyofundishwa na walimu wao wa somo la sayansi kuhusu moyo wa binadamu unavyofanya kazi, katika mahafali ya saba ya darasa la saba shuleni hapo, eneo la Ihumwa jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake wachagizwa kushiriki uchaguzi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WANAWAKE wametakiwa kujitokeza katika uchaguzi mkuu 2020, kuwachagua viongozi wenye maono ya kuwaunganisha katika fursa mbalimbali za kiuchumi zilizoko ndani na nje ya nchi.

Akizungumza jana kwenye Jukwaa la 'Mwanamke Shujaa Tanzania', Mwenyekiti wa Jukwaa hilo Dodoma, Peris Privatus, alisema ikiwa wanawake watakubali kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo, watachagua na kuwapa nafasi viongozi wenye ndoto za kuwajengea mbinu za kuingia kwenye uchumi wa viwanda.

Mwenyekiti huyo alisema ili kufika kilele cha mafanikio kwa pamoja wanawake wanapaswa kusaidiana kuzifikia ndoto za kila mmoja wao.

"Wanawake wajasiriamali tuna nafasi kubwa katika jamii yetu ya Tanzania na dunia nzima kwa ujumla. Tuna wajibu wa kuwahamasisha wanawake wenzetu kujituma na kukubali mafanikio.

Kwa kuanza tumeleta bidhaa zetu hapa kuonyesha wanawake wenzetu kuwa ni wakati wa mafanikio ya wanawake, hakuna kubaki nyuma," alisema Privatus.

Katibu wa Jukwaa hilo, Emeryciana Mbulagwisha, alisema baadhi ya wanawake hawajapata ujasiri wa kuishi kwa kufuatana na matakwa yao.

"Katika mafanikio ya kila mwanamke tunahimiza nguvu ya mwanamke katika jamii tukiamini wanawake wote wanaweza kuchukua nafasi hii kutambua ujasiri na upambanaji wao katika jamii," alisema.

Aliongeza kuwa jukwaa hilo lingependa kuona kila mwanamke anapewa kipaumbele na kuwezeshwa katika jamii, jambo litakalosababisha wengi kujitambua na kufanya mambo makubwa zaidi na kutambulika kimataifa.

"Mwanamke mpambanaji ni mwanamke imara na anayeijua nguvu iliyo ndani yake ya kupambana na kukabiliana na changamoto katika nyanja mbalimbali za maisha ili kutimiza malengo yake," alisema Mbulagwisha.

Tumaini Kyando, mjasirimali mwanamke katika jukwaa hilo, alisema licha ya wanawake kukabiliana na changamoto nyingi, wanapaswa kuongeza juhudi bila kuchoka.

Kyando aliongeza kuwa ili kuwa na wanawake wengi mashujaa lazima kuongeza zaidi ujasiri katika nafasi za kujiendeleza na kuinuana bila kuoneana wivu wa maendeleo .

Several Joseph, alisema mwanamke jasiri haogopi kushindwa na changamoto zilizo mbele yake, hivyo siku zote huchagua kuzikabili.

Alisema wanawake wengi wajasiri wamefanikiwa kuinua uchumi wao na kuzisimamia familia zao wakati mwingine bila hata ya msaada wa mwanamume.

"Kila mwanamke mpambanaji ana ndoto za kuwa mtu fulani ama kufikia malengo fulani, hivyo basi hatupaswi kuogopa kuwa tofauti na mategemeo ya wengine," alisisitiza.

# Waomba ajira za walimu wasaidizi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kutenga bajeti kwa ajili ya kuajiri walimu wasaidizi wa watoto wenye ulemavu mchanganyiko wakiwamo viziwi wasioona ili kusaidia kupata elimu.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la kimataifa la Sense Tanzania (Sense International Tanzania), Naomi Lugoe, aliyasema hayo jana katika kikao cha kuwasilisha taarifa ya Mradi wa Elimu Jumuishi kwa Watoto hao, uliofanyika kwa miaka minne kwenye mikoa ya Dar es Salaam na Kilimanjaro.

Mradi huo umefanyika kuanzia Juni, 2016 hadi Mei, mwaka huu kwa ufadhili wa Mfuko wa Ubunifu kwa Maendeleo ya Watu (HDIF), ulioanzishwa na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la Misaada la Uingereza (UKAID).

Mkurugenzi huyo alisema kwa kipindi hicho shirika hilo limewaingiza darasani watoto 100 wenye ulemavu mchanganyiko wakiwamo viziwi wasioona.


"Kila mtoto ana haki ya kujifunza na lazima apewe mazingira ya kumwezesha kujifunza kwa hiyo kwa watoto wenye ulemavu mchanganyiko wanatakiwa kuwa na msaidizi ambaye atamsaidia mwalimu katika kile anachofundisha,"alisema.

Alisema katika utafiti wao wa miaka mine, wamebaini kama watoto hao wakiwa na wasaidizi watafanikiwa kujifunza vitu darasani.

"Hawa watoto 100 kupitia utaratibu wa kuwa na mwalimu msaidizi imesaidia wao kujifunza na hata wazazi wamekuwa ni mashahidi kuona watoto wao wana mabadiliko fulani. Elimu hasa wanayopewa awali kabisa ni stadi ya maisha, kutambua vitu kwa kutumia alama mguso ambapo mwalimu anafundisha na msaidizi anamsaidia yule mtoto kuelewa kinachoendelea darasani," alisema.

Akifungua kikao hicho, Mkurugenzi wa Elimu Maalum kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Magreth Matonya, alishukuru shirika hilo kubuni uwapo wa mwalimu msaidizi ili kuwasaidia watoto viziwi wasioona kupitia lugha mguso.

"Shirika hili limeweza elimu jumuishi maana huko kwenye jamii watu wanasema kiziwi kutoona hawezi kusoma wala kukaa darasani, hawezi kuelewa kwa sababu lugha anayoitumia inaitwa lugha mguso. Lakini Sense wamekuja na kitu cha tofauti kwamba wana nafasi kubwa ya kujifunza kupitia mwalimu msaidizi," alisema.





# Waziri ataka ulinzi watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Shadya Mohammed Suleiman, amewataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawalinda watoto wao wakati wote hasa nyakati za usiku.

Aliyasema hayo juzi alipomtembelea mtoto Abdul-rauf Tibawahid Fadhil, mkazi wa Mpapa, Zanzibar, aliyelazwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, baada ya kupewa vidonge ambavyo havijajulikana na mtu asiyemjua alipotumwa dukani majira ya usiku.

Shadya alisema si jambo jema watoto kuwatuma dukani majira ya usiku na hali hiyo inaweza kuwahatarishia maisha yao na watu wabaya ambao hawana dhamira njema.

Pia alisema serikali inathamini watoto kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kielimu ili waweze kujitambua, kujielewa na kuwa wataalamu wa baadaye.

Naibu Waziri huyo alisema wazazi wanapaswa kukubali kuwa walimwengu hivi sasa wameharibika hivyo ni vyema kuwa makini katika kuwatunza watoto wao wakati wote.

"Japo tunakwenda kwa wakati wa sayansi na teknolojia, turejesheni utamaduni na maadili yetu. Watoto ikifika saa 12:00 jioni tuhakikishe wamo ndani, hii itatufanya tuwaepushe na majanga mbalimbali hasa ya kudhalilishwa," alisema.

Shadya aliviomba vyombo vya sheria kuhakikisha mtu huyo anachukuliwa hatua zinazostahiki ikiwemo kufikishwa mahakamani na wizara haipo tayari kufumbia macho kitendo hicho ambacho ni cha kinyama kilichofanywa na mtuhumiwa huyo.

Naye, mjomba wa mtoto huyo Mwadini Ame Mwadini, aliviomba vyombo vya sheria kumchukulia hatua mtu aliyefanya tukio hilo, ili mtoto wake apate haki.

Sambamba na hayo aliishauri serikali kuweka mikakati juu ya watu wanaofanya uhalifu wa aina hiyo kwa sababu wanaopoteza muelekeo wa watoto kwa kuwafanyia vitendo vibaya ikiwemo udhalilishaji wa kijinsia.

Mtoto Abdulrauf alisema alitumwa dukani akanunue kibiriti pamoja na vocha ya simu na wakati akielekea huko dukani alikutana na mtu asiemfahamu na kumlisha vidonge saba vya dawa.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki ambapo tayari vipimo vya damu vya mtoto huyo vimeshachukuliwa kwa ajili ya uchunguzi, ili kubaini vidonge alivyopewa na mtuhumiwa huyo ni vya aina gani.

# 'Viongozi wa dini hubirini amani'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa dini wametakiwa kuhubiri amani hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib, alisema jana hayo mjini hapa wakati akizungumza katika kongamano la amani kwa ajili ya uchaguzi mkuu. Kongamano hilo limeandaliwa na uongozi wa makanisa ya Anglikana Zanzibar na kanisa la kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKT) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mufti wa Zanzibar.

Alisema Tanzania inatarajia kufanya uchaguzi mkuu, hivyo ni vyema viongozi wa dini wakahubiri amani ili kupunguza mihemko ya kisiasa na taifa kuendelea kubaki salama kabla na baada ya uchaguzi.

"Hiki ni kipindi kigumu cha kuelekea uchaguzi mkuu, hivyo amani kwanza mengine baadaye maana kuna maisha baada ya uchaguzi," alisema Mkuu wa Mkoa huyo. Alisema Tanzania imetokomeza ugonjwa wa corona kutokana na ibada walizokuwa wanafanya wananchi kutokana na dini zao. Kwa mantiki hiyo, alisema ni vyema kuendelea kufanya ibada ya kuiombea nchi amani ili kufanya uchaguzi kwa usalama bila kukwaruzana.

"Nimefurahishwa na uamuzi wenu wa kutayarisha kongamano kubwa kama hili lenye ujumbe wa kuliombea dua taifa la Tanzania kufanya uchaguzi mkuu kwa amani na utulivu," alisema Khatib. Naye Askofu wa Anglikana Dayosisi ya Zanzibar, Dk. Michael Hafidh, alisema taifa la Tanzania tangu lilipoasisiwa mwaka 1964 wananchi wake wamekuwa wakiishi katika mazingira ya amani na utulivu hatua ambayo imesaidia kukua kwa uchumi na ustawi wa jamii.

"Wezetu nchi za nje wakisikia milio ya risasi na mabomu, wanakimbia lakini sisi Watanzania tukisikia milio hiyo tunaikimbilia ili kutaka kuona kuna jambo gani kwa sababu si kawaida yetu kuwa na machafuko. Mungu aendelee kutulinda na amani idumu milele," alisema.

Aliviomba vyombo vya dola kutekeleza wajibu wao wa kudumisha amani na kuwalinda marais wa nchi ili wawe salama dhidi ya matukio ya shari na vurugu za kisiasa.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mufti wa Zanzibar, Sheikh Khatib Mziwanda, aliwaomba viongozi wa kisiasa kuchunga ndimi zao katika kipindi hiki muhimu ambacho taifa linapita ili kuwawezesha wananchi kuchagua viongozi kwa njia ya kidemokrasia.

Aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kuzingatia kanuni za masharti ya uchaguzi ambayo wametia saini ikiwa ni mkataba wa kuhakikisha wanashiriki katika uchaguzi mkuu huku na kudumisha amani.

"Viongozi wa vyama vya siasa nchini kafanyeni kampeni zenu za uchaguzi mkuu huku mkiweka kipaumbele suala la amani na utulivu kwa sababu kuna maisha baada ya uchaguzi," alisema.

Mkuu wa Upelelezi kutoka Jeshi la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Obasi Nguvule, alisema wamejipanga vizuri kulinda amani na utulivu pamoja na mali za raia ikiwa ni moja ya majukumu makubwa ya jeshi hilo kwa mujibu wa katiba.

Aliwataka wanasiasa kutumia uwanja wa siasa kwa ajili ya kutoa sera za vyama na na uchaguzi usitumiwe kwa ajili ya kugawa wananchi.




Naibu Katibu Mkuu Chama cha ACT-Wazalendo Zanzibar, Nassor Ahmed Mazurui, akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake, Vuga Zanzibar juzi, kuhusu mapingamizi waliyowekewa wagombea ubunge wa chama hicho. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanaswa kwa tuhuma za kuomba, kupokea rushwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) inawashikilia watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Mkuu wa ZAECA katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ali Seif, aliwataja watu hao kuwa ni Ramadhan Khamis ambaye ni mhasibu msaidizi na Khatib Mohammed Juma ambaye ni mhasibu wa halmashauri hiyo.

Alisema watu hao kwa pamoja wanatuhumiwa kuomba rushwa ya Sh. 300,000 na kufanikiwa kupokea Sh. 100,000.

Seif alisema watuhumiwa hao kwa pamoja walikamatwa Agosti 24, mwaka huu, majira ya saa 5:00 za asubuhi katika maeneo ya Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja.

"Tumefanikiwa kuwakamata watu hao baada ya kupata taarifa kutoka kwa mlalamikaji na ZAECA iliweka mtego ambao ulifanikisha kuwakamata," alisema.

Seif alisema kosa hilo ni kinyume na kifungu cha 36 cha sheria namba moja ya mwaka 2012 ya sheria za ZAECA.

Alisema Agosti 21, mwaka huu, mlalamikaji alilipwa fedha zake za kuchimba kisima cha halmashauri hiyo kilichoko Jambiani Mbuyuni, ambazo ni mfuko wa jimbo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya wananchi katika jimbo la Paje.

Baada ya kumlipa fedha zake, alisema watuhumiwa hao waliomba kupatiwa kiasi cha fedha hizo.

Sambamba na hayo, alitumia fursa hiyo kuwataka watumishi wa umma katika taasisi mbalimbali za serikali kufuata taratibu na sheria za kazi ili kujiepusha kuingia matatani.

Aidha aliwataka wale wote wenye malalamiko dhidi ya watuhumiwa hao wafike katika mamlaka hiyo ili wapeleke malalamiko yao na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria.



WEMA

UKURASA 12

Nipashe
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI AGOSTI 29, 2020



## ATAINGIA HIVI!

# Harmonize Wiki ya Wananchi

ATATOKA VIPI? Ni swali ambalo wanajiuliza wapenzi wa Yanga na mashabiki wa muziki kwa msanii anayetamba hivi sasa Harmonize pale atakapingia uwanja wa Benjamin Mkapa, kutumbuiza kilele cha Wiki ya Wananchi.

Kilele cha tamasha la Yanga, linalojulikana kama Wiki ya Wananchi itakuwa Agosti 30, hapo Staa huyo atawachezesha wapenzi wa soka mirindimo ya kijeshi.

Hata hivyo, Harmonize, amejaribu kunogesha kwamba amejipanga kuingia tofauti na si kama alivyoingia bosi wake wa Zamani Diamond Platnumz, ambaye aliingia uwanjani hapo kwa kutumia chopa.

Harmonize hajaweka bayana ataingia hapo kwa kutumia usafiri gani, lakini wengi wanatabiri itakuwa 'sapraizi' ya nguvu kuwa kutoka.

Hata hivyo, amewataka mashabiki wake kutomchukulia vibaya pale atakapoingia na kuwarusha watu, kwani suala la ushabiki wa soka sawa na dini, hubeba watu wa aina tofauti.

"Mimi ni mwananchi timu yangu ninayoishabikia ni Yanga, kwenye michezo na hakuna hisia ngumu kwamba nikishangilia timu fulani eti mashabiki wangu wajigawe pia mpira sio vita, nia yetu ni kuusogeza mpira mbele wala sio uadui, ila ninachowaahidi siku ambayo nitashuka pale uwanja wa Mkapa hamtaamini" amesema Harmonize.

BASI SAWA

## Wema wamekushtukia janja yako

WAMEMSHTUKIA! Ni kama wameshtukia jambo baada ya mwigizaji staa wa filamu nchini, Wema Sepetu, kumuandikia ujumbe mzito mchezaji mpya wa Carlinhos Carmo10.

Ujumbe wa Wema, ulimtaka mwanandinga huyo kuwapa ubingwa Wanayanga, na baadae ndio wataanza kuongea lugha nyingine.

"Tunachotaka sisi mpate ubingwa tena mara saba alafu ndo tuanze kuongea lugha moja na zitabaki saba hivyo hivyo maana ubingwa ni wetu round hii karibu sana, halafu nasikia harufu ya mechi mechi hivi karibuni au ni mimi tu, nataka tupate mechi moja bwana, au unasemaje Engineer Makini" ameandika Wema Sepetu

Kama vile kashtukia dili, Steve Nyerere, naye akachangia kwa kuandika,"Umeanza, huyo kijana anajua mpira tu, nakujua unaanzaga hivi hivi kujifanya mlezi wa wana hahahahahahahahah tutakupiga wallah uchelewi mchwitiiiiiiii huyu.




## Aslay kawa mbogo, yeye anadunda!

AMECHARUKA! Mwanamuziki wa Bongo Fleva, Aslay, amekuja juu akitaka baadhi ya vyombo vilivyoripoti kuwa yeye amefariki kuchukuliwa hatua za kisheria.

Aslay ameiomba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania TCRA, kuvichukulia hatua baadhi ya mitandao baada ya kumzushia kwamba amefariki dunia.

Inasikitisha na kushangaza sana unawezaje kumzushia mwanadamu mwenzako kifo na mabaya mengi, wanaofanya hivi ni Watanzania wa kawaida kama sisi ambao tulitamani watupe habari na burudani na wao wapate riziki, lakini wako bize kutupotosha na hata kuharibu majina yetu" Ulisema baadhi ya manene katika ujumbe alioposti kwenye ukurasa wake wa Instagram.





## Jux atamani tabasamu la Vanessa

MWANAMUZIKI mkali wa miondoko ya RnB, Juma Jux, anafanya shoo ya aina yake, baada ya kuandaa burudani ya kipekee kwa ajili ya wanawake pekee.

Hata hivyo, penzi lake na msanii mwenzake Vanessa Mdee, bado halijayeyuka kwani amesema angepata furaha kama angemuona mrembo huyo akimshuhudia siku hiyo.

"Kiukweli ningetamani uwepo wake maana nimewaambia watu wangu waalike wanawake wote ambao wapo kwenye hii Industry, naamini Vanessa Mdee ni mtu ambaye yupo kwenye Industry ila nilisikitishwa na taarifa zake za kuacha muziki japo sio kwa ubaya, pia naamini atakuwa hayupo kama angekuwapo ningetamani nimkaribishe sina tatizo naye," amesema

## Mapito Yangu: Ukewenza kaa la moto

MWANAMUZIKI Marijani Rajab aliwahi kuimba kuwa ukewenza ni fahari ya wanaume, lakini kwa wanawake ni tabu. Ni jehanamu na ni kaa la moto.

Filamu ya 'Mapito Yangu' inaakisi jambo hilo. Ni filamu inayoonyesha kuwa wakati mwingine wanawake wanapokuwa wameolewa na mwanaume mmoja, kila mmoja atajitahidi kuonyesha mapenzi, au kitu chochote ambacho mume atadhani ni zaidi ya mwenzake.

Katika hali hii baadhi ya wanawake wanajikuta wanatumia mbinu halali na chafu ili kuonekana wapendwe zaidi. Inapotumika mbinu chafu, ndipo balaa huzuka wakati mwingine kwa familia nzima.

Imechezwa na Angel Nicholous, Abdallah Vicent, Kasele Ramadhani, Aisha Hamisi, Munira Hamisi, Samira Hamisi, Zakia Yakubu, Zuberi Shaaban na wengineo.

Inaanza kuonyesha Zubeda akiwa kwenye gari, ghafla mbele anajitokeza mwanamke anayezuia barabara. Anasimama na kumfuata. Mwanamke yule anataka kumkumbatia akisema 'Zubeda mwanangu'. Zubada anamtambua. Lakini badala ya kukubali kukumbatiwa, anaanza kumtukana na kumtolea maneno machafu na kuelekea kwenye gari yake, akaondoka.

Siku ya pili mwanamke yule alifika kwenye nyumba ya Zubeda na kupokelewa na rafiki zake ambao walimpa chakula. Zubada aliporejea, alimkuta mwanamke yule na kukipiga teke chakula na kumtimua. Zubeda aliwaambia rafiki zake kuwa yule ni mama yake mkubwa, lakini visa alivyovifanya huko nyuma, vilisababisha familia yote kusambaratika, ndiyo maana hataki hata kumuona.

Miaka mingi nyuma, mzee Zuberi alikuwa na wake wawili, Munira mke mkubwa na Aisha mke mdogo. Munira alizaa mtoto wa kiume aliyeitwa Fadhili na Aisha alizaa mtoto wa kike, Zubeda.

Mke mkubwa mama Fadhili alitumia mbinu chafu ili mwenzake aonekane ni mbaya ndani ya nyumba. Ubaguzi wa mtoto wa kike na kiume nao ulitumika, kwani mama Fadhili alikuwa akimtumia mtoto wake wa kiume



Fadhili ili kumuumiza mwenzake ambaye ana mtoto wa kike Zubada.

Lengo linatimia, mama Zubeda na binti yake wanatimuliwa kwa mzee Zuberi na kubaki mama Fadhili pekee.

Fadhili anafanya uhuni shuleni, anafukuzwa. Anaporudi nyumbani anaanza kuwa mlevi, kitu ambacho kinafanya baba yake kujinyonga.

Zubeda anapata bahati anaolewa na mwanaume tajiri. Ndipo siku moja mama Fadhili anakutana na Zubeda na kufanyiwa mabaya yale. Anachofanya Zubeda ni kulipiza kisasi jinsi alivyofanyiwa miaka ya nyuma na mama yake mkubwa.

Mama Zubeda anapata habari kuwa mke mwenzake alikuja pale akiwa amechoka, lakini binti yake alimfukuza.

Roho ya huruma inamjia mama Zubeda, akamwambia binti yake asifanye hivyo tena. Mama Fadhili anaitwa kwenye nyumba ya Zubeda. Anakutana na mke mwenzake. Anamuomba msamaha. Yameisha na kuanza tena maisha mapya. Wanalishana keki kwa sababu ni siku ya kuzaliwa kwa mama Zubada.





## Mjomba Fujo awaambia 'Magufuli anatosha'

MTUNZI na msanii wa nyimbo za miondoko ya kughani, George Paul Mzelu, maarufu kama 'Mjomba Fujo' amekamilisha kurekodi video ya wimbo wake mpya unaoitwa 'Magufuli Anatosha'.

Wimbo huo umeanza kusikika kupitia vituo vya radio, luninga na mtadao wa kijamii wa Yutube.

"Ndani ya wimbo huo, kumeangaliwa kila mafanikio ambayo nchi imefikia ikiwa chini ya Rais John Pombe Magufuli, hapo utapata kuwa anastahili kupewa dhamana tena ya kuiongoza Tanzania" amesema.

Ameongeza katika mashairi ya wimbo huo kuwa, hakuna ambacho rais Magufuli amekiacha katika kusimamia utendaji wa kila sekta na hilo ndilo lililoifanya Tanzania kufikia hatua ya uchumi wa kati.

## BENDI ZILIZOPAA HARAKA, ZIKAFA GHAFLA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Bendi za African Stars 'Twanga Pepeta, FM Academia na TOT Plus zilitamba miaka ya 2000, kulikuwa na bendi kadhaa ambazo ziliitwa ndogo.

Hata hivyo bendi hizo hazikudumu kwa muda mrefu, zikafa kifo cha mende huku kukiwa na maswali mengi kwa mashabiki wa muziki wa dansi nchini Tanzania.

Wengi hawakuamini kama zilikufa vifo vya kawaida, badala yake haikuaminika kuwa bendi hizo zilizojizolea mashabiki zingevunjika wakati wanazihitaji.

Baadhi wakaamini kuwa huenda kulikuwa na mkono wa bendi kubwa kuhakikisha bendi hizo hazidumu ili zenyewe ziendelee kutawala muziki. Hizi ndizo bendi zilizotesa na kuchengua mashabiki kwa muda mfupi tu kisha zikatoweka.

**Chuchu Sound**

Hakuna shabiki yoyote yule ambaye atakataa kuwa moja ya bendi zilizoanza kuwa tishio kwenye utawala wa bendi kuwa ni Chuchu Sound. Ilikuwa ikiongozwa na mwanamuziki Yusuph Chuchu ambaye ni marehemu kwa sasa.

Alilitengeneza kundi dogo, lakini lilitisha kwa kupiga muziki wa dansi la kawaida, lakini pia lenye mahadhi ya mduara. Hasa ilijulikana kwa mduara, huku ikiwa na wanamuziki waliokuwa wakichombeza maneno yaliyowakuna mno mashabiki kama 'Bwa'n Chazz tam', na 'eeeh kwa kheri, yaliyokuwa yakisemwa na Chuchu mwenyewe na Omari Mkali. Hata hivyo bendi hiyo ilikufa ghafla na kuwatia simanzi mashabiki wengi ndani na nje ya Jiji.

**Pamo Sound**

Bendi hii iliundwa baada ya Chuchu Sound kuvunjika, ikiwa na baadhi ya wanamuziki wa Chuchu Sound, pamoja na Akudo Impact. Haikutofautiana sana upigaji na Chuchu na hata vionjo vya mduara.

Kilichotokea, afadhali hata ya Chuchu Sound ilidumu, hii ndiyo ilivunjika mapema zaidi.

**Mokibo Sound**

Bendi hii ilikuwa na maskani yake maeneo ya Mabibo jijini Dar es Salaam. Ilikusanya baadhi ya wanamuziki nyota kutoka bendi mbalimbali kubwa na ndogo, Watanzania na hata kutoka Congo DR.

Lakini nayo haikudumu muda mrefu. Ilirekodi nyimbo zake mara moja tu na pamoja na kukonga nyoyo za mashabiki wengi wa muziki lakini ikavuniika.

**Mchinga Sound**

Ni bendi iliyoanza kwa kishindo zaidi na kukusanya wanamuziki wengi kutoka African Stars 'Twanga Pepeta', wakiwamo kina Adolf Mbinga, Rogat Hegga 'Katapila' na hiyo ndiyo bendi iliyomtambulisha rasmi kwenye ulimwengu wa muziki, Mwinjuma Muumini.

Ila afadhali hii ilidumu kidogo na kutoka kibao vingi vilivyopendwa na kuwa maarufu sana.

Kama kawaida, bendi hii nayo ilikufa na karibuni wanamuziki wake wengi wachukuliwa na African Revolution 'Tamtam', ambayo ni bendi dada na Twanga Pepeta.

**Beta Musica**

Inajulikana zaidi kwa kibao chao cha 'Bana Beta' ambacho ndicho kiliibeba zaidi bendi hiyo. Ilikuwa na wamuziki wengi kutoka Congo DR. Wengi walikuwa ni wale waliojiengua kutoka Diamond Sound, FM Academia na hata Acudo Impact.

Ilivuma kwa muda mfupu tu na kusambaratika, kila mwanamuziki akienda anakokujua mwenyewe.



**Mchinga Sound**



# Mehdi hukujua wanawake sumu?

MWANAMUZIKI wa Iran, Mehdi Rajabian, amejikuta katika mikono ya dola baada ya kukiuka sheria ya kujumuika na Wanawake.

Mwanamuziki huyo, mwenye miaka 30 ambaye alishawahi kufungwa gerezani mara mbili, amekamatwa baada ya kuimba na kucheza na wasanii wa kike.

Wizara ya utamaduni na miongozo ya Uislamu haijaongelea lolote kuhusu suala hilo.

Mwanamuziki huyo aishie mjini Sari, Kaskazini mwa Iran, amesema kuwa alitwa na vikosi vya polisi tarehe 10 mwezi Agosti, ambao walimkamata na kumpeleka mahakamani.



## Taji la B.I.G lapigwa mnada

TAJI lenye historia katika muziki wa hiphop nchini Marekani, lililovaliwa na Notorious B.I.G. siku chache kabla ya kifo chake limepigwa mnada.

Biggie alivalia taji hilo siku tatu kabla ya kupigwa risasi hadi kufa mnamoMachi 9,  1997. Msanii huyo wa muziki wa kufoka foka na mpiga picha wake, Barron Claiborne waliitia saini wakati huo. Barron amekuwa akimiliki tangu wakati huo.

”Nafurahi sana kugawana taji hili la kihistoria na umma”, amesema.

## Halima ukisikia manungayembe ndo hao

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood, Halima Abubakar, ametoa ushauri kwa wanawake wenzake kuvunja uhusiano na wanaume wenye tabia ya  udhalilishaji wa kijinsia.

Katika ujumbe wake wa Istagram, Halima, amesema haivumiliki kuona mwanaume anabadilisha wanawake kama nguo, ikiwa yeye ana mpenzi wake.

“Usilalamike pale mtu anapowarukia wanawake mmoja hadi mwingine, wakati mwingine unahitaji kuwa na mwanamume mwingine, ni muhimu kuwaacha kwani hakuna mwanamke mwenye matatizo ya akili,” amesema Halima.





## Kevin mbona hukusema una Covid 19?

MCHEKESHAJI staa wa Marekani, Kevin Hurt, amesema alipata maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19 mapema mwaka huu.

Kulingana na mtandao wa PageSix, msanii huyo ambaye amepata umaarufu kutokana na shoo zake, amesena suala hilo hakuweza kulizungumza mapema, lakini ukweli alikuwa muathirika wa virusi hivyo vya corona.


“Tatizo ni kwamba niliugua kipindi ambacho alikuwa anaugua Tom Hanks,na nisingeweza kusema kitu chochote kwa sababu yeye alikuwa na mashabiki wengi kuliko mimi,” amesema Hurt

## Omotola yamkuta tena

HABARI mbaya! Mashabiki wa mwigizaji mkongwe wa Nollywood, Omotola Jalade Ekeinde , wiki hii wamekuwa na wasiwasi baada ya msanii huyo kugundulika ameambukizwa virusi vya Covid 19.

Omotola, ametumia ukurasa wake wa Instagram, kuwataarifu mashabiki wake kwamba amepata vipimo vua corona na majibu yanaonyesha amepata maambukizi.

“Hello mashabiki wangu, najua mtashangazwa na haya ninayowaambia, nilikuwa naumwa na sasa naendelea vizuri na baada ya vipimo vinaonyesha nina Covid 19...lakini sasa nipo vizuri,” amesema Omotola.



MAKALA

# GEL: Fursa kwa vijana kujiajiri zipo wakiamua

Na Mwandishi Wetu

VIJANA nchini wanaweza kujiajiri na kuajiri wenzao baada ya kupata elimu ya vyuo vikuu badala ya kulialia kusubiri ajira kwani fursa za kuwawezesha kufikia ndoto zao ziko kila upande.

Mwandishi wa makala hii amezungumza na Mkurugenzi wa Global Education Link, Abdulmalik Mollel ambaye anaelezea namna vijana wanavyoweza kuchangamkia fursa mbalimbali za biashara zilizopo kwa kuanza kuwa wakala wa kampuni.

Mollel ambaye taasisi yake inafanyakazi ya kuwaunganisha wanafunzi Watanzania na vyuo vikuu vya nje ya nchi alitoa mawazo hayo alipokuwa akizungumzia maandalizi ya kuwakutanisha wanafunzi waliosoma vyuo vikuu mbalimbali nje ya nchi kwenye mahafali ya pili Septemba 19, mwaka huu.

Anasema hivi karibuni wanatarajia kuwakutanisha vijana 400 waliosoma vyuo vikuu mbalimbali nje ya nchi kuwatengenezea daraja na fursa kwao kupata fursa mbalimbali za uwekezaji na namna wanavyoweza kutumia ujuzi wao kujiajiri na kuajiri vijana wenzao.

Anasema kwa kuwa kampuni na taasisi mbalimbali zinakuwa kwenye mahafali hayo kuna uwezekano wa kuanzisha biashara zao kwa kuwa mawakala wa kampuni kubwa kama wanavyofanya wafanyabiashara kutoka nchi mbalimbali.




Mkurugenzi Mkuu wa GEL, Abdulmalik Mollel akiwa na wanafunzi wanaokwenda kusoma vyuo vikuu nchini China mwaka jana.

Anasema kwasababu vijana wanaosoma nje ya nchi wamepata fursa ya kuzoea mazingira ya mataifa hayo wanaweza kuitumia kama fursa ya kufanyabiashara kama watawezeshwa hata mtaji modogo.

"Inawezekana kuna mtu anataka msambazaji au mwenza wa biashara sasa wakija pale ndani mfano Mohamed Enterprises anazalisha bidhaa nyingi za chakula akatokea kijana akamwambia mwekezaji kwanini usinipe mafuta yako nikasambaza mkoa flani anaweza kuwa wakala tu na akafanya biashara nzuri," anasema

Anasema kuna wafanyabiashara kutoka mataifa mbalimbali ambao wamekuwa mawakala wa kampuni kubwa kwa kuagiza bidhaa wanazozalisha na kuuza bidhaa zao hapa nchini na wamekuwa wakifanya vizuri sana kwenye masoko.

"Tunawaona wachina wanakuja hapa nchini si wenye viwanda ni mawakala tu wa viwanda lakini tunawaona wanaagiza kontena mbili au tatu za tiles na mwisho wa siku ana kontena 100 au 200 huo mtazamo huo vijana wanaujua kwani hata hao tunawaita wawekezaji wakubwa siyo wakubwa, wenye viwanda wako huko nje sasa tunataka kuwakutanisha vijana wajadili haya," anasema

Anasema lengo la mahafali hayo ni kuhakikisha wanafunzi Watanzania waliosoma nje ya nchi hawarudi kimya kimya na kinyonge kwani wao ni wazalendo walioamua kuacha fursa zilizoko huko baada ya masomo yao na kuja kuijenga nchi yao.

Mollel anasema wahitimu hao waliaminiwa na taifa na ndiyo sababu walipewa viza za kwenda kusoma nje ya nchi kwaajili ya manufaa yao familia zao na kwaajili ya nchi yao hivyo kurudi kwao ni kurejesha furaha nyumbani kwani wanatarajiwa kutoa mchango mkubwa kwa nchi.

Anasema GEL itawakutanisha wanafunzi hao kwaajili ya kujenga mtandao na taasisi na watu mbalimbali hapa nchini baada ya kukaa nje ya nchi kwa muda mrefu ambako huko walishajenga aina nyingine ya maisha.

"Mfano mtoto ameenda huko akiwa na miaka 17 amekaa huko miaka minne au sita anarudi amekuwa mtu mzima amekuta mambo mapya sasa akifika akikosa timu kama aliyokuwa nayo kule anakata tamaa sasa kitendo cha kumkutanisha mtu aliyekuwa Uingereza, India, China, Canada au Afrika kusini kwenye jengo moja ni jambo kubwa sana na la msingi," anasema Mollel

Aidha, Mollel anasema wanafunzi hao wakikutanishwa wataona kama milango ya maisha yao imefunguliwa kwani watatengeneza mtandao mpya na wenzao waliomaliza nao mwaka mmoja kwenye vyuo hivyo nje ya nchi kwasababu awali hakukuwa na mahafali ya aina hiyo.

Kwa mujibu wa Mollel, mahafali hayo ni fursa kwa wahitimu hao kwani kuna kampuni mbalimbali ambayo yametoka kwenye nchi mbalimbali ambazo wanafunzi hao walisoma ambazo zitakuwa zinatafuta wataalamu wa fani wanazozihitaji hivyo wakikutanishwa itakuwa na manufaa kwao.

"Kuna wawekezaji ambao wanatafuta watu waliosoma kwenye nchi zao angalau wenye kujua lugha zao kidogo sasa hii ni nafasi ya kuwaita hawa kwamba nani amewekeza nini na anahitaji vijana wataalamu sasa ukiwakutanisha ni fursa kubwa sana kwa wawekezaji na vijana," anasema Mollel

Alisema kuna taasisi za serikali kama menejimenti ya utumishi wa umma na ile ya kutafutia watu ajira ya Taesa wanahitaji rasilimali watu ambazo zipo lakini hakuna daraja lililowakutanisha hivyo mahafali hayo ni daraja la kuwaunganisha wahitimu hao na taasisi hizo.

Anasema taasisi hizo za serikali na za binafsi zitakaposhiriki kwenye mahafali hayo zitapata kujua orodha ya wanafunzi waliosoma fani mbalimbali wanazohitaji hivyo kutengeneza daraja baina ya pande hizo mbili na kuondoa malalamiko kwamba kuna uhaba wa wataalamu na vijana kulalamikia tatizo la ajira.

Mollel anasema inawezekana kabisa kuna fursa za ajira lakini kwa bahati mbaya kukakosekana wataalamu wa wanaotakiwa kwa wakati huo hiyo hivyo taasisi hizo zitakapohudhuria mahafali hayo zitachukua baadhi ya vijana wahitmu wataaluma mbalimbali kwenda kufanya nao kazi badala ya kuagiza wataalamu kutoka nje.

Anasema mahafali hayo ni jukwaa kwa serikali pia kutumia wanafunzi hao kuitangaza nchi kwenye nyanja mbalimbali ikiwemo elimu na utalii kwa wanafunzi wenzao wa nje ya nchi hivyo kuvutia vyuo kuja kuwekeza nchini na kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo.




Mfanyakazi wa GEL akiwakagua wanafunzi viambatanisho vyao muhimu kabla ya kwenda masomoni.

# OTA BENGA

## ■Mwafrika aliyepitia magumu Marekani
## ■Aliishi na nyani na kuwekwa maonyesho

Na Mwandishi wetu

KIJANA shupavu, mwenye ngozi nyeusi inayong'ara na kuashiria ni zao halisi la Kiafrika.

Pamoja na kuzaliwa katika eneo lenye utajiri wa madini na misitu mikubwa, Ota Benga hakuweza kuona tena mandhari ya bara lake na nchi yake anayoipenda, badala yake maisha yake yalibaki kuwa machungu na udhalilishaji wa kutisha.

Ota Benga, ambaye sasa habari zake zimefichuka na kushtua dunia, alizaliwa katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), baadae mwaka 1904 alipelekwa Marekani kama mtumwa, huko aliwekwa katika mbuga ya wanyama kama onyesho.

Kulingana na mwandishi Pamela Newkirk, ambaye ameandika habari nyingi kuhusu kijana huyo, anafichua kwamba kuna matukio kadhaa yalifichwa kwa zaidi ya miaka 100.

**KUTEKWA MISITU YA CONGO**

Kuibuka kwa picha yake baada ya karne moja kupita, kumeibua hisia kali kutokana na machungu aliyopitia na sasa watu wanahitaji ukweli kuhusu kijana huyo.

Picha ya kijana wa Kiafrika katika eneo la kutunzia nyani ndani ya bustani ya Wanyama ya Bronx, mji wa New York, imeleta hoja mpya kuhusu maisha yake yaliyojaa huzuni na masikitiko.

Hata hivyo, picha hiyo ya Ota Benga, iliyopigwa mwaka 1906 kwenye onyesho, imesababisha Shirika la kuhifadhi Wanyama pori kuomba msamaha.

Hatua inayokuja baada ya maandamano yanayoendelea nchini Marekani, baada mauaji ya George Floyd na kuanza tena kuangalia namna ubaguzi wa rangi unavyotokea nchini humo.

Cristian Samper, Rais wa Chama cha Uhifadhi wa Wanyama Pori, anasema ni muhimu kuakisi historia ya hifadhi hiyo na ubaguzi wa rangi katika taasisi zao.

Aliapa kuishinikiza bustani ya wanyama ya Bronx, kuhakikisha inakuwa na uwazi kuhusu kile kilichotokea kuanzia Septemba 9, 1906 siku moja baada ya Benga, kuonyeshwa kwenye onesho, hadi alipoondolewa kwenye bustani hiyo. Septemba 28, mwaka 906.

**MATESO YALIYOFICHWA**

Shirika hilo la uhifadhi wa wanyama pori limejihusisha katika kuficha ukweli kwa karne nzima.

Muda wote lilishindwa kuzungumzia kile ambacho kilitokea kwa mwanamume huyo mweusi.

Mapema mwaka wa 1906, barua kutoka kwa hifadhi hiyo, ambayo ilipatikana inaonyesha ikijitetea kwa kuandika uongo kuzima ukosoaji kwa kueleza Benga alikuwa mfanyakazi wa hifadhi hiyo.



Picha iliyowakasirisha watu wengi ya Ota Benga akiwa na nyani katika onyesho

**OTA BENGA NI NANI?**

Alikamatwa Machi 1904 na mfanyabiashara wa Marekani, Samuel Verner, katika mizitu ya DRC, wakati huo ilikuwa ikifahamika kama Congo ya Ubelgiji.

Hata hivyo, umri wake haujulikani, inakisiwa wakati anakamatwa na kutekwa alikuwa na miaka 12 au 13

Alisafirishwa kwa meli hadi New Orleans na baadae mwaka huo, kuwekwa kwenye maonesho ya dunia yaliyofanyika huko St Loius akiwa na vijana wengine wanane wa Kiafrika.

Katika kazi yake hiyo ya kuwafurahisha wazungu kama bidhaa, aliwekwa katika eneo la wazi katika miezi ya baridi bila kupewa nguo za kujikinga wala malazi mazuri.

September 1906, aliwekwa kwenye maonesho kwa siku 20 katika bustani ya wanyama ya Bronx huko New York na kuwa kivutio cha wengi kufika katika eneo hilo.

Hata hivyo, aliondolewa hapo baada ya mawaziri wa Kikristo kuonyesha hasira zao na kutaka aachiwe huru, na hapo ndipo alipohamishwa na kupelekwa katika nyumba ya kulea yatima weusi ya Howard, huko New York. Kituo hicho kilisimamiwa na mchungaji Mmarekani Mweusi, James H Gordon.

Januari 1910, aliendа mji wa Lynchburg, katika Seminari ya kitheolojia kwa ajili ya wanafunzi weusi huko.

Akiwa huko, Benga aliwafunza wavulana wenzake walioishi jirani namna ya kuwinda,kuvua samaki na kuwasimulia mambo mengi yaliyotokea nyumbani kwao kabla ya kutekwa na wazungu.

Inasemekana Benga aliathiriwa na ugonjwa wa sonona kutokana na kukumbuka nyumbani kwao. Machi 1916 alijipiga risasi kwa bunduki ambayo alikuwa ameificha. Inadhaniwa wakati huo alikuwa na umri wa karibu miaka 25.

**SIRI YAFICHUKA**

Baada ya kifo chake, makala ya gazeti la New York lilijaribu kutoa siri kuhusu maonesho yake.

"Kazi hii ndio chanzo cha kujulikana kwa taarifa ambayo ilikuwa iliyofichwa na hifadhi ya wanyama pori kuwa alikuwa akishikiliwa kama mmoja wa waliokuwa wakiwapa faida kwenye maonyesho kwa kukaa kwenye kizimba cha nyani. Makala hayo yameeleza.

**HISTORICAL SOCIETY**

Makala hayo ilikinzana na zingine ambazo zilizotolewa miaka kumi ya mwanzo katika magazeti mbalimbali nchini humo na Ulaya.

Gazeti la New York Times, pekee lilikuwa limechapisha taarifa kadhaa kuhusiana na suala hilo, moja wapo ikiwa ni Septemba, 9 1906, ambayo kichwa cha habari kilikuwa: " Bushman Shares A Cage With Bronx Park Apes". Yaani 'Mtu wa porini aishi na nyani kwenye kizimba kimoja kwenye hifadhi ya Bronx'

Kisha, mwaka 1974, William Bridges, mtunzi wa hifadhi hiyo alidai kwamba huenda kile hasa kilichotokea kisifahamike.

Kitabu kilichochapishwa 1992 na mwandishi mwenza kiliandika kuwa, alikuwa mjukuu wa Samuel Verner, mwanamume aliyekwenda Congo, akiwa amevalia mavazi ya kijeshi kumteka Ota Benga na wengine kwa ajili ya maonesho ya dunia mwaka 1904 huko St Louis.

Katika moja ya magazeti tangu kuchapishwa kwa kitabu hicho, lilionyesha kwamba kijana Verner alidai kuwa Benga alifurahia kuwa kama onesho huko New York.

Hifadhi hiyo ya wanyama sasa imeweka taarifa mtandaoni miongoni ikiwa ni barua zenye taarifa za

Pamela Newkirk, alipopata fursa ya kutembelea eneo ambapo Benga alikuwa amefanywa kuwa onesho, jengo hilo limefungwa kuzuia watu kulifikia.

"Tunasikitika kwamba watu wengi na vizazi vimeumizwa kwa matendo haya au kwa kushindwa kwetu kukemea kitendo hicho hadharani na kwa wakati ufaao." Alisema bosi Samper.

**BBC**



Ota Benga wakati akiwa na umri kati ya 13 na 14

# Uganda kuomba Mungu waponywe corona

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ametangaza siku ya Jumamosi, kuwa ya kitaifa kwa ajili ya maombi maalum kupambana na Covid-19.

Katika ujumbe wake kupitia mitandao ya kijamii, kiongozi huyo, alisema wazo la kuwepo kwa siku ya maombi lilitoka kwa raia wake ambaye alimtaja kuwa na maono kutoka kwa Mungu.

"Mungu alikua amemwambia katika moano kuwa ninapaswa kuandaa maombi, yaandaliwe kisayansi, ili Mungu atuponye na Covid-19," alisema Museven.

Aliendeleea kwa kusema "Ninatangaza tarehe 29 Agosti, 2020, kuwa siku ya maombi ya kitaifa na siku ya mapumziko kwa umma. Kaeni majumbani mwenu au kwenye viwanja vya nyumba zenu na muombe," Uganda ilirekodi visa 2,679 vya watu wenye maambukizi ya virusi vya coronana na vifo 28.

Serikali iliweka masharti ya kudhibiti maambukizi baada ya kuthibitisha kisa cha kwanza mwezi Machi. **BBC.**



Mwanamke akilia mbele ya mwili wa mtu aliyeuawa na polisi karibu na makazi ya watu masikini mjini Sao Carlos, kufuatia operesheni maalum ya kupambana na magenge ya wauzaji wa dawa za kulevya inayoendeshwa jijini Rio de Janeiro, nchini Brazil. **(PICHA: REUTERS)**

# Wakimbizi wa Burundi warejea

**BUJUMBURA, Burundi**

KUNDI la wakimbizi 493 limewasili nchini Burundi jana, baada ya kuishi nchi jirani ya Rwanda kwa muda mrefu.

Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiya, aliwakaribisha raia hao na kuelezea furaha yake baada ya kurudi katika nchi yao na kuwahakikishia kuwasaidia kurudi katika maisha yao ya awali.

Wakimbizi hao ni kundi la kwanza kati ya wakimbizi 72,000 waliokimbilia Rwanda mwaka 2015, kufuatia ghasia zilizotokea baada ya uchaguzi wa mwaka 2015.

Watu 6,000 kati yao wamekuwa wakiishi katika kambi ya wakimbizi ya Mahama, iliyopo mashariki mwa Rwanda huku wengine wamewekwa katika kambi iliyopo mijini Kigali na Huye, kulingana na Shirika la Umoja wa mataifa la wakimbizi UNHCR.

Walipowasili walipokelewa na Waziri wa mambo ya ndani wa Burundi, Gervais Ndirakobuca, na Waziri wa Afya, Dkt Thaddée Ndikumana.

Katika ujumbe wake wa Twitter, Rais Ndayishimiya aliwakaribisha na kusisitiza serikali yake itawapatia ushirikiano.

"Karibu ndugu zetu waliotoka ukimbizini Mahama. Nifuraha kubwa kwa familia zao na kwa Burundi. Wahusika wanaombwa kuwasaidia katika mchakato wa kurejea katika maisha ya kawaida. Tunawataka na wengine wanaotaka kurejea warudi, Burundi ni yetu sote. Karibu kwenu pazuri!", aliandika Ndayishimiye katika ujumbe wake wa Twitter. **BBC.**

# Trump amshambulia Joe Biden

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amemshambulia mpinzani wake, Joe Biden, kuwa ameingia katika siasa kwa bahati mbaya na kwamba atahatarisha usalama wa Marekani.

Trump, aliyasema hayo wakati akikubali uteuzi wa chama chake cha Republican, katika hotuba aliyoitoa akiwa katika Ikulu ya nchi hiyo ya White House juzi.

Kiongozi huyo anakabiliana na madai ya kukaidi mwongozo wa mapambano dhidi ya virusi vya corona na kusababisha taifa hilo kupoteza watu 1,000 kila siku.

Pia anakabiliwa na hali ya mtafaruku wa ubaguzi, kuporomoka kwa uchumi na dharura ya kiafya ya taifa. Trump alitoa mtazamo wa ushindi na matumaini kwa hali ya baadae ya Marekani, lakini alisema matumaini hayo yanaweza kupatikana iwapo atamshinda Biden ambaye ni mgombea wa chama cha Democratic. Biden anaongoza katika kura za maoni katika majimbo muhimu. **DW.**

# Rais wa zamani wa Mali aachiwa huru

**BAMAKO, Mali**

RAIS wa zamani wa Mali, Ibrahim Boubacar Keita, amerejea nyumbani chini ya ulinzi mkali, baada ya kuachiwa huru na wanajeshi waliopindua serikali yake.

Kuachiwa huru kiongozi huyo, kunafuatia shinikizo kali kutoka kwa mataifa 15 wanachama wa ECOWAS, ambao walitaka Keita kuondolewa kuzuizini.

Kulingana na familia ya rais huyo wa zamani, Keita alirejea nyumbani juzi jioni, baada ya kushikiliwa kwa siku 10 na wanajeshi walioasi na kuipundua serikali wiki iliyopita.

Keita mwenye miaka 75, alijiuzulu muda mfupi baada ya kuondolewa madarakani.

Aliyekuwa rais wa Nigeria, Goodluck Jonathan, ambaye anahusika katika mazungumzo na wanajeshi walioasi, alisema kuachiwa kwa Keita kunaonyesha wanajeshi hao wanajaribu kutekeleza matakwa ya Jumuiya ya ECOWAS, ili kuepuka vikwazo.

Jumuiya hiyo ya ECOWAS ilitarajiwa kukutana jana kujadili mikakati mipya ya kuchukua katika mgogoro huo wa Mali.

Moja ya matakwa hayo inawataka wanajeshi wanaoiongoza Mali waweke mara moja serikali ya mpito na kuandaa uchaguzi baada ya angalau mwaka mmoja ili kurejesha utawala wa kiraia.

Hata hivyo, wanajeshi hao wanaojiita 'Kamati ya kitaifa ya ukombozi wa watu wake' imependekeza kukaa madarakani kwa muda wa miaka mitatu kwa kueleza inafanya hivyo kutokana na masuala ya usalama kufuatia mashambulizi ya makundi ya wanamgambo katika upande wa Mali ya kati na upande wa Kaskazini. **DW.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba ya Gorofa 1, inauzwa na fremu za biashara, umeme na maji. Inafaa kwa kuishi kwa na biashara. **Mawasiliano: 0757 079057.**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PETER ALBERT HOWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 236 DPJ** aina ya **Toyota IST.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi

**MBE/MBE/RB/626093/2020**

115877602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MWANAIDI ADADI RAJABU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba ya usajili **T793 DKE** iliyotolewa na mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:

**DAR/MAG/RB/560697/2020**

115877002

**AMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;230/2020**

**Ombi la MAISARA AHMED MUMBA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ANNA ENOCK MWAIPOPO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 4/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/08/2020.

Tarehe 14/08/2020

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU

115876802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo ya CHAMWINO - MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 62 /2020.**

**Ombi la KELVIN RAYMOND KOSHUMA kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu RAYMOND JONATHAN KOSHUMA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 03/08/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe 16/07/2020

HAKIMU

MAHAKAMA YA MWANZO

CHAMWINO MJINI

DODOMA.

115877302

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO CHA UMILIKI**

Mimi **MWANAHAJI THABIT – S.L.P 178** Tanga nikiwa mtu mzima na akili zangu timamu naapa na kuthibitisha mbele ya hakimu mahakamani ifuatavyo;

1. Kwamba mimi **MWANAHAJI THABIT** ni mmiliki wa kiwanja Na 199 kitalu "c" High Density kwanjeka area Tanga city **TAN/RB/6I8207/2020**
2. Kwamba, nimepotelewa na hati ya kiwanja Na 199 kitalu "c" high density Kwanjeka area Tanga city na nimeitafuta pasipo matumaini ya kuipata tena na kwa uthibitisho nimefika polisi na kupata loss report
3. Kwamba, kwa kiapo hiki naomba ifahamike kuwa mimi **MWANAHAJI THABIT** ni mmiliki halali wa kiwanja hicho Na 199 kitalu "c" high density kwanjeka Tanga

**UTHIBITISHO**

Mimi **MWANAHAJI THABIT** nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapa kwanzia aya ya 1-3 ni ukweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sharia ya viapo (The oaths and statutory declaration sAct. Cap.34 R; E 2002 ).

Imethitishwa hapa Tanga

MWANAHAJI THABIT

Leo tarehe ..........

Mbele ya ..........

Cheo ..........

Anwani ..........

Sahihi ..........

..........

Sahihi ya muapaji

115876902

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**JOYCE MANYAMA MATESI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA **BAJAJI** AINA YA **REAR** YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 993 BTZ** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI

**KAH/RB/1302/2020**

115877502

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# Mauaji Harusini-27

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango,**

**0716 350534)**

Ndipo Eddy alipokumbuka maneno ya Shani kuwa ana matatizo makubwa ambayo alihitaji kumsimulia.

"Usinione hivi Eddy, mimi nimekuwa na matatizo makubwa. Na hadi leo bado nina matatizo makubwa. Na sikuwa na mtu yoyote wa kushea naye matatizo yangu. Wewe ni rafiki yangu, naomba tuwe pamoja kwenye furaha na matatizo yangu.

Nitakwambia, lakini siyo hapa. Nitakwambia sehemu maalum. Tukiwa wawili tu."

Anachojua yeye kuwa Shani ni msichana ambaye amejikuta amepoteza wazazi wake wote wawili. Baba yake ni tajiri, hivyo Shani anatarajia kurithishwa mali zote za baba yake. "Je kuwa wafanyabiashara wakubwa waliokuwa washirika wa baba yake ambayo baada ya kumuua Patiyo, wanataka wamteketeze na binti yake wa pekee? Je kwa nini wasitumie bastola kama walivyomuua baba yake tajiri na mwenye ulinzi ambaye wamemuua 'kitemi' zaidi, kwa nini watake kumuua binti mnyonge asiyekuwa na uwezo wowote hata wa kujilinda kidhaifu na kwa woga zaidi?" Eddy alichanua mambo na akili yake ikamwambia kuwa huenda waliomuua baba yake Shani, aitwaye Patiyo na mkewe waliokuwa wakitoka kufunga naye ndoa, ambaye Eddy alikuwa ni Shangazi yake aitwaye Grace, si watu walewale.

Kitu cha kwanza alichoona kinaweza kumfanya apate mwanga zaidi ni kuonana na Fikiri kwanza.


"Ndiyo. Yeye ndiye atasema nani aliyemtuma na ndiye atatoa mwanga kama ni yeye mwenyewe ndiye alitaka kufanya hivyo au la." Kitu kimoja ambacho Eddy hakutaka kufanya ni kumfahamisha Shani kuhusu jaribio lake la kutaka kuuawa kwa sumu. Hakutaka kwa sababu ingemtisha na kuanza kuishi kwa wasiwasi.

Alitaka kwanza ajue kwa nini na ni nani aliyefanya vile, amtie mbaroni ndiyo Shani afahamu njama hizo.

"Ni lazima nimkakamate mtu huyu anayetaka kumuua mpenzi wangu. Na inawezekana ikawa ni chanzo cha kujua juu ya kifo cha shangazi yangu Grace na mumewe Patiyo waliuawa masaa kadhaa baada ya kutoka kufunga ndoa." Eddy aliapa.

**********************************

Mvua ilinza kunyesha kwa nguvu na ilidumu kiasi cha dakika 15 hivi na




kusababisha eneo la Kigogo Fresh kuwa na madimbwi ya maji ya hapa na pale.

Ilikuwa ni saa sita usiku hivi, eneo hilo likiwa na watu wachache sana. Fikiri alikuwa mmoja wa watu wachache waliokuwa kwenye eneo hilo.

Alikuwa ametoka kwenye moja ya baa na tayari alikuwa chakari kwa ulevi. Siku hiyo hakwenda kazini.

Alitoka nyumbani saa nne asubuhi, akaenda kwa demu wake Halima ambako alikula chakula cha mchana, wakaongozana hadi baa. Walipotoka hapo walikwenda moja kwa moja hadi nyumba ya wageni na walipomaliza mambo yao, alimsindikiza nyumbani.

Baada ya kuhakikisha kuwa amefika salama, alikuwa akirejea nyumbani kwa mkewe.

Kwa siku za karibuni hakuwa na furaha hata chembe. Alikuwa amepoteza kifuko chake cha sumu.

Pamoja na kwamba tayari alikuwa ameshamaliza kazi ya kumuwekea Shani kwenye chakula, lakini hakujua ni kwa vipi kifuko kimepotea.

"Nimekiangusha wapi?" Alijiuliza mara kwa mara. Wakati mwingine alianza kuwa na wasiwasi.

Wazo lingine lilimuondoa kwenye wasiwasi kuwa huenda kifuko hicho kilianguka mfukoni wakati akiwa amekaa kwenye kiti cha basi.

Wasiwasi wake ni kwamba sumu ile isidondokee maeneo ya kazini kwake, kwenye hoteli ya ABC, kwani uongozi unaweza kuwa na wasiwasi na kuchunguza kwa nini kipo pale na kwa nia gani.

Alijipongeza kwa kazi aliyoifanya ya kutia sumu kwenye chakula cha Shani na alikuwa na uhakika kuwa baada ya miezi mitatu mpaka sita, binti yule mrembo angetoweka kwenye uso wa dunia.

Moyoni alihuzunika kumpoteza binti kama yule, tena yeye akiwa ameshiriki kumfanyia ubaya.

Kwanza ni mteja wake aliyemzoea, tena wakati mwingine akimuachia chochote kitu akitaka kuondoka.

Pili ni mmoja kati ya mabinti warembo aliyepata kuwaona kwenye umri wake, tena akiwa bado msichana mbichi.

Alimpenda sana Shani, ila alijua hata akidhikiri usiku kucha, hawezi kumpata msichana kama yule, mrembo na tajiri pia.

"Pesa kitu kibaya sana." Alijiambia mwenyewe.

Pesa ndiyo ilimfanya kukubali kupewa sumu na kuiweka kwenye chakula ili demu yule afe taratibu.

Hakujua hata dhamira ya waliomtuma kazi hiyo ni nini?

Alichojua yeye ni kwamba ametumwa kazi hiyo ambayo kwake ilikuwa ni ndogo tu kama ilivyokuwa, lakini akilipwa kiasi cha shilingi milioni mbili.

Tayari alikuwa ameshapokea bahasha ya shilingi milioni moja kutoka kwa Jim na ndugu zake.

Na sasa alikuwa anasubiri tena kiasi kama hicho, kwani aliahidiwa akishamaliza kazi.

Kesho asubuhi ndiyo ilikuwa siku ya yeye kwenda maeneo ya Kinondoni Studio ili kuchukua bakshishi yake.

Kwa kawaida Fikiri alikuwa mzoefu mno na pombe. Hata akilewa vipi, huwa hayumbi wala kupoteza kumbukumbu.

Alifika kwenye kona moja ya kichochoro chenye urefu wa mita 30 hivi, kabla ya kutokea kwenye mtaa ambao unakwenda nyumbani kwake.

Hatua mbili tu kabla hajafika kwenye kona, alihisi kitu kama kivuli au mzimu hivi.

Alisita kidogo. Alichelewa. Kitu kizito kilitua kichwani na kusababisha ayumbe. Kabla hajajua nini kimetokea, alipigwa na kitu kingine kizito kichwani kilichomsababishia maumivu makali.

Pigo la tatu hakulisikia sana, kwani tayari kumbukumbu zilianza kupotea kichwani. Alikuwa kama mtu ambaye anataka kulala usingizi mzito. Pigo la nne hakulisikia. Tayari alikuwa marahemu.

**************************************

Jim na ndugu zake Paul, George na Ben hawakuwa tayari kutoa kwa mara ya pili kiasi cha shilingi milioni moja kwa Fikiri.

Waliona ile milioni moja ya kwanza inamtosha sana. Baada ya kuwaletea taarifa kuwa ameshafanya kazi aliyotumwa ya kumuwekea sumu Shani kwenye chakula, waliona haifai aendelee kuishi.

Si pesa tu, lakini pia ili kwao iwe salama waliona ni lazima Fikiri naye afe kabla hata Shani hajafariki.

Ingawa waliamini plani yao ya kumuua Shani taratibu kiasi cha kuwafanya polisi washindwe kujua sumu ile alikula nini na wapi, lakini hawakutaka mtu yoyote atie shaka.

Walichofanya ni kumtafuta kibaka mmoja ambaye alipew kiasi cha shilingi laki moja tu, akaifanya kazi hiyo.

Mapigo manne ya magongo kichwani, yalimfanya Fikiri atangulie mbele za haki.

Hata mtu aliyetumwa, hakumfahamu kabisa mtu aliyemtuma, kwani alikuwa mgeni machoni mwake.

Na hata siku aliyokuwa akimpiga na gongo kichwani, alikuwa akishuhudia ili kuhakikisha kazi hiyo inafanyika, hadi alipothibitisha kuwa Fadhili hatoinuka tena milele.

Mpango huo ulisimamishwa na George ambaye ndiye aliyekuwepo kwenye eneo la tukio.

Mpango wa kuhakikisha Shani anafariki na mali zote za marehemu baba yake Patiyo kuingia mikononi mwa ndugu hao ulionekana kuwa unaanza kufanikiwa kwa kiwango cha kuridhisha.

**************************************

Magazeti mengi hayakuipa uzito mkubwa habari hiyo. Ilionekana kama vile mlevi mmoja ameuawa na walevi wenzake akitoka kwenye baa.

Wengine walisema walikuwa wakigombea demu. Wapo waliosema alifumwa na mwanamke wa mtu. Kila mmoja aliongea lake.

Uzito wa mauaji yake yalikuwa maeneo ya Kigogo nyumbani kwake ambako watu wengi walikusanyika.

Kazini kwake nako hoteli siku hiyo ilifungwa. Kila mteja aliposikia habari hiyo alisikitika.

Wengine walieleza siku moja kabla ya kifo walivyokutana na kuongea.

Ni mtu mmoja tu aliyeipa uzito wa hali ya juu mauji yake. Ni Eddy Kamal. Alikuwa anasoma gazeti na kurudia tena. Akacheka. Alijua kabisa kifo cha Fikiri hakikuwa cha kawaida.

Wala hakugombea demu, kufumaniwa, au kukutana na vibaka njiani.

Pamoja na kuwapa pongezi watu waliofanya kitu hicho, lakini aliona kama wamefanya kosa kubwa sana la kiufundi.

Ni Fikiri huyo huyo ambaye aliangusha kifuko kwa bahati mbaya kwenye hoteli ya ABC na alipokiangalia kilikuwa ni cha sumu.

Akapatwa na wasiwasi na chakula kilicholekwa na mhudumu huyo kwa Shani. Akakipeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Vipimo vilionyesha kuwa mabaki wa chakula yalikuwa na sumu ile ile ambayo alikuwa ameiokota, ilipoanguka kwenye mfuko wa Fikiri.

Wakati Eddy akiwa anatafakari sababu ya yote yale na hatimaye kuazimia kumsaka Fikiri, leo inakuja kuonekana kuwa ameuawa.

Aliwaza kuwa vyovyote itakavyokuwa, Fikiri atakuwa ameuawa na watu waomtuma kumuwekea Shani sumu.

Hapo ndipo alipogundua kuwa wasiwasi wake ulikuwa sahihi. Na hata maneno ya Shani kuwa ana matatizo makubwa ni sahihi pia. Eddy alijua kuwa nyuma ya pazia kuna mpango kabambe unaosukwa kuhakikisha kuwa binti yule ambaye kwa sasa ni mpenzi wake anapoteza maisha "Sababu ni nini?" Alijiuliza bila kupata jibu.

Kingine alichogundua kuwa huenda anachofahamu Shani ni kidogo tu cha mpango mzima unaosukwa juu yake.

Akagundua kuwa kumbe yupo mikononi mwa mrembo Shani kwa sababu maalum.

"Nakupenda sana Shani. Nitakusaidia." Alijikuta akiongeza kwa sauti peke yake.

***Itaendelea Jumamosi***

# WAJUMBE

## WAMKATA DROGBA URAIS WA FIF

**ABDIJAN, Ivory Coast**

KAMATI ya uchaguzi ya Shirikisho la Soka la Ivory Coast (FIF), imemuengua mchezaji wa zamani wa Chelsea, Ddier Drogba, kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi wa urais wa shirikisho hilo.

Nyota huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya Ivory Coast, Drogba, ameondolewa kwenye uchaguzi huo kwa sababu ya nyaraka zake kukosa vigezo vilivyotakiwa ambavyo hata hivyo havikutajwa.

Kwa mujibu wa BBC Sport, Drogba alikuwa akipewa nafasi kubwa zaidi ya kushinda kwenye uchaguzi huo wa FIF unaotarajiwa kufanyika Septemba 5, mwaka huu.

Kuenguliwa kwa Drogba sasa kunafanya wabaki wagombea wawili wa nafasi hiyo ya urais.

Wagombe waliobaki kuwania nafasi hiyo ni Sory Diabate na Idriss Diallo.



Drogba

## UNITED YAMFUATA FATI WA BARCELONA

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United ipo tayari kulipa pauni milioni 153, ili kuipata saini ya nyota kinda wa Barcelona, Ansu Fati ajiunge na kikosi hicho.

Ripoti zinaeleza kuwa, winga huyo mwenye miaka 17, atakuwa mbadala wa nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, ambaye dau lake linatajwa kuwa pauni milioni 108.

Fati amecheza jumla ya mechi 33 kwenye mashindano yote ndani ya Barcelona msimu uliopita na alitupia jumla ya mabao nane.

United inahitaji saini yake kwa kuwa bado ni kinda, hivyo wanaamini atakuwa na faida kubwa akitua ndani ya kikosi hicho.

Barcelona bado haijafikiria kumuacha kinda huyo kwa kuwa amekuwa akipata malezi akiwa chini ya staa wa timu hiyo, Lionel Messi ambaye inaelezwa kuwa anahitaji kuondoka ndani ya timu ya Barcelona.

Sancho ambaye ni winga pia msimu uliopita alihusika kwenye jumla ya mabao 40 akifunga 20 na kutoa pasi za mwisho 20.

## RONALDO AJIPANGA UBORA ZAIDI JUVE

**TURIN, Italia**

MALENGO ya Cristiano Ronaldo ni "kuwa bora zaidi nchini Italia, Ulaya na duniani" akiwa na Juventus msimu wa 2020-21.

Juve licha ya kuwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Italia msimu wa 2019-20, lakini walijikuta wakiangukia pua kwenye Kombe la Coppa Italia na kutolewa hatua ya 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kipigo cha Ulaya kutoka kwa Lyon mapema Agosti kikamfanya kocha Maurizio Sarri kupoteza kazi yake, huku Andrea Pirlo akichukua mikoba ya kukinoa kikosi hicho.

Ronaldo alifunga mabao 37 kwenye mashindano yote katika msimu wake wa pili na Bianconeri, na sasa amebainisha kwamba anajipanga kwa ajili ya msimu ujao.

"Kwa uhakika nipo tayari kwa ajili ya msimu wa tatu na Bianconeri, ari na molari yangu ni kubwa sana," aliandika Ronaldo kwenye ukurasa wake Instagram.

"Malengo, ushindi, kujituma, kujitoa na weledi pamoja na nguvu zangu kuwasaidia wachezaji wenzangu kwa ajili ya Juventus, tutafanya kazi bora ili kuwa bora Italia, Ulaya na duniani!

"Kuvunja rekodi, kuvuka vizuizi, kushinda mataji na kufanikisha malego yangu binafsi, kufanya vizuri zaidi kwa mara nyingine. Kufikia juu na kufanikisha kuzikabili changamoto zote."

Msimu mpya wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, utaanza Septemba 19, mwaka huu.



HABARI MICHEZO

# SARR ATUA RASMI CHELSEA




**LONDON, England**

CHELSEA imekamilisha usajili wa mlinzi, Malang Sarr, kutoka Klabu ya Nice inayoshiriki Ligi Kuu ya Ufaransa.

Sarr ametua Chelsea kwa mkataba wa miaka mitano na kuwa mchezaji wa nne kusajiliwa katika dirisha hili kubwa la kipindi cha majira ya joto.

Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 21, raia wa Ufaransa alikuwa mchezaji huru baada ya mkataba wake na Nice kumalizika mwishoni mwa Juni, ambapo Chelsea wamemsajili lakini ataendelea kuwa nje kwa mkopo msimu ujao wa 2020-21.

Sarr ameshaitumikia timu ya Taifa ya Vijana ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 21 na amecheza jumla ya mechi 119 akiwa Nice akifunga mabao matatu.

Anakuwa mchezaji wa nne kutua Stamford Bridge baada ya Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 27, kutoka Ajax, Timo Werner kutokea RB Leipzig na Ben Chilwell aliyetoka Leicester City.

Mkurugenzi wa michezo wa Chelsea, Marina Granovskaia, amesema: "Nafasi ya kumsajili sarr hakuna timu hata moja ambayo ingeiacha.

"Ni kijana mwenye kipaji kizuri kikiendelezwa vema kwa siku za usoni, tutakuwa tunamuangalia kwa makini akiwa sehemu nyingine msimu ujao."

## POGBA AONDOLEWA UFARASA KWA CORONA

**PARIS Ufaransa,**

KIUNGO wa mshambuliaji wa Manchester United, Paul Pogba, amekutwa na maambukizi ya virusi vya corona, kocha wa timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps, amethibitisha.

Pogba mwenye umri wa miaka 27, sasa amewekwa karantini kwa siku 14 kabla ya kuungana na wenzake.




Paul sasa ameondolewa kwenye kikosi cha Ufaransa kilichokuwa kimetajwa kucheza dhidi ya Sweden Septemba 5, na mtanange wa nyumbani dhidi ya Croatia siku tatu baadaye.

Hata hivyo, nyota huyo anaweza kuwa sehemu ya mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya England wakati timu yake ya Man United itakapocheza na Crystal Palace, Septemba 19 pale Old Trafford.

Pogba nafasi yake imechukuliwa na kinda wa Rennes ya Ufaransa, Eduardo Camavinga.



## ARTETA MATUMAINI KIBAO KWA AUBAMEYANG KUSAINI

**LONDON, England**

MIKEL Arteta anaamini Arsenal inakaribia kufikia makubaliano na Pierre-Emerick Aubameyang juu ya mkataba mpya.

Aubameyang, ambaye alifunga mabao 29 katika mashindano yote kwa Arsenal msimu uliopita, amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa pale kwenye viunga vya dimba la Emirates.

Hata hivyo, mazungumzo juu ya mkataba mpya kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, yanaendelea, na Arteta - ambaye kikosi chake kitaikabili Liverpool kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii Jumamosi - anaimani mkataba huo utasainiwa hivi karibuni.

"Nimeendelea kuwa na mtazamo chanya," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Tumekuwa na mazunguzo mazuri na yeye pamoja na wakala wake na nina jiamini tutafikia makubaliano hivi karibuni. Hizo ndio hisia zangu."

Arteta, ambaye pia anakaribia kumsajili mlinzi wa Lille, Gabriel Magalhaes, katika kikosi chake, anajua kwamba mkataba mpya utaongeza molari ya Aubameyang kwa klabu.

"Kwa uhakika kabisa, na kwa upande wake yeye," alisema Arteta.

"Nafikiri anatakiwa kuwa na furaha kubwa kama akiweza kubaki katika klabu hii kwa muda mrefu. Nafikiri watu watafurahia habari hizi."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KOEMAN AMTULIZA GRIEZMANN BARCA

●●●Kwa hakika kabisa alitaka kuondoka, alijiona hayupo kwenye mipango ya klabu hiyo, na...

**BARCELONA, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Antoine Griezmann alitaka kuondoka pale Camp Nou kabla ya kuzungumza na kocha mpya, Ronald Koeman, amedai wakala wake wa zamani, Eric Olhats.

Griezmann alikabiliwa na msimu wa kwanza mgumu pale Barca baada ya kuhamia hapo kwa euro milioni 120 akitokea kwa wapinzani wao wa LaLiga, Atletico Madrid, akishindwa kuonyesha kiwango cha juu licha ya kufunga mabao 15 kwenye mashindano yote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alihusishwa na kwenda Paris Saint-Germain, huku ukurasa wa mbele wa gazeti la Marca la jana Ijumaa likiripoti kwamba, Atletico imekataa mpango wa Barca wa kumbadilisha Griezmann na Joao Felix.

Olhats, ambaye awali alikuwa mwakilishi wa Griezmann, alidai kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alikuwa anataka kuondoka kabla ya Barca kumteua Koeman kuchukua nafasi ya Quique Setien.

"Kabla ya kipigo cha 8-2 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Bayern Munich, Griezmann alikuwa tayari na mpango wa kuondoka Barcelona," alisema Olhats akiiambia RMC.

"Ukweli ni kwamba, Griezmann alijiona hayupo kwenye mipango ya klabu hiyo, na hakupenda kuendelea katika hali hiyo.

"Kwa hakika kabisa alitaka kuondoka. Halafu kilichotokea ni kwamba alifanya majadiliano na Koeman na kumhakikishia nafasi yake.

"(Koeman) alimuelezea mipango yake, na alimwambia kwamba yeye ni mchezaji muhimu sana kwa kikosi hicho."

Griezmann alifunga mabao tisa katika mechi 35 za mashindano yote aliyoichezea Barca wakati wakiachia Kombe la Ligi Kuu kwenda kwa wapizani wao, Real Madrid.

Pia alifunga mara mbili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na walitolewa na Bayern Munich kwenye hatua ya robo fainali.

## KWA UFUPI

**MESSI, GUARDIOLA WATETA**

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, amewasiliana na Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola na kumfahamisha kwamba anataka kuondoka Barcelona. ***(Times)***

**RONALDO AITULIZA JUVE**

NYOTA wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 35, amezima tetesi kuhusu mustakbali wake kwa kusema kwamba anajiandaa kwa msimu wa tatu pale Juventus. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**HAVERTZ AKARIBIA CHELSEA**

KLABU ya Chelsea iko katika hatua za mwisho kukamilisha usajili wa kiungo mshambuliaji wa Ujerumani, anayekipigia Bayer Leverkusen, Kai Havertz mwenye umri wamiaka 21. (Guardian)

**ZLATAN, MILAN WAMALIZANA**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 38, amekubali mkataba mpya wa mwaka mmoja kubakia AC Milan. Mkataba huo unaaminika kuwa na thamani ya pauni milioni sita. ***(Sky Sports Italia)***

**MAN CITY YAMKOMALIA MESSI**

MANCHESTER City inajiandaa kuipa Barcelona kitita cha pauni milioni 89.5 pamoja na Garcia, kiungo wa Kireno Bernardo Silva mwenye miaka 26 na mshambuliji wa Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 23, kwa ajili ya kumnasa Messi. ***(Sport)***

**MADRID YATAJA BEI YA SERGIO**

REAL Madrid inataka euro milioni 20, kwa ajili ya beki wake wa kushoto raia wa Hispania, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 23, ambaye amezivutia klabu za Manchester United, Tottenham, Juventus na Inter Milan wakati akicheza kwa mkopo Sevilla. ***(Marca)***

**AURIER KUTIMKA SPURS**

KUWASILI kwa mlinzi wa kulia raia wa Ireland, Matt Doherty mwenye umri wa miaka 28 katika timu ya Tottenham kutoka Wolves, kunaweza kuwa tiketi ya mlinzi wa Ivory Coast, Serge Aurier mwenye miaka 27, kuondoka. ***(Standard)***

**SPURS YAIKATALIA MILAN**

KLABU ya Tottenham imekataa ofa ya kwanza kutoka AC Milan kwa ajili ya Serge Aurier, huku Bayer Leverkusen ikionyesha nia ya kutaka huduma ya mlinzi huyo mwenye miaka 27. ***(Sky Sports)***

**UNITED YAMUWANIA TONALI**

KLABU ya Manchester United imewasilisha ombi la kumnasa kiungo wa Brescia, Sandro Tonali mwenye umri wa miaka 20, ambaye anatajwa kama mmoja wa makinda wanaokuja juu nchini Italia. ***(Corriere dello Sport via Metro)***

**ANGELINO CHAMBO YA MESSI**

KLABU ya Manchester City inaweza kuwatoa mabeki wake raia wa Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19 na Angelino mwenye miaka 23, kama chambo ili kumnasa Messi, kama hawatamsajili akiwa mchezaji huru. ***(Mail)***

**LEEDS YAMTAKA FELIPE**

LEEDS United inajiandaa kupeleka ombi la kumnasa beki wa kati wa Brazil anayekipiga Lazio, Luiz Felipe, mwenye umri wa miaka 23.

HABARI MICHEZO

# SIMBA QUEENS YASAJILI NYOTA WA YANGA PRINCESS, MLANDIZI

**Na Saada Akida**

BAADA ya mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba, kukamilisha usajili wa kikosi chao, hatimaye jana mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake, Simba Queens, nao walifunga usajili msimu huu kwa kumsainisha kiungo mshambuliaji wa Mlandizi Queens, Philemena Daniel.

Mratibu wa Simba Queens, Seleman Erassy, aliliambia gazeti hili kuwa, kufanikiwa kwa usajili huo kumetokana na Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Mohammed "Mo" Dewji, kufanyia kazi mapendekezo yao waliyoyatoa.

Alisema mbali na nyota huyo, tayari wameshawasajili Shelda Boniface kutoka Yanga Princess, Asha Shabani kutoka Kigoma Sisterz, Koku Ally mchezaji huru na Omita Berth Odhiambo kutoka Kisumu All Stars ya Kenya.

"Ni kweli tulikutana na Mo Dewji na kumueleza mikakati na mahitaji yetu ya kuboresha timu, kuhusu usajili hilo limekamika na tayari tumesajili wachezaji ambao watatusaidia katika ligi na michuano ya kimataifa ambayo tutacheza," alisema Erassy.

Alisema kuhusu kuboresha benchi la ufundi tayari wamekubaliana na Sofia Mseti kutoka kituo cha JK Parks ambaye ni kocha msaidizi, lakini pia wapo katika mchakato wa kutafuta mwalimu wa makipa.

"Tupo imara katika maboresho yetu na kikosi chetu kimeonekana ubora wake msimu uliopita ambapo tumetwaa ubingwa tukiwa na mechi mkononi, bado tunahitaji kuendelea kutwaa mataji, hivyo tunaboresha kikosi ili kuwa imara zaidi," alisema Erassy. Hivi karibuni Mo, aliliambia gazeti hili kuwa alikutana na viongozi wa Simba Queens likiwamo benchi la ufundi na kujadiliana mambo mbalimbali mojawapo likiwa kuliongezea nguvu benchi hilo pamoja na kuimarisha kikosi cha mabingwa hao.

"Tayari nimezungumza na viongozi wa Simba Queens, kila kitu kimeenda vizuri hasa katika usajili wetu, lakini pia kuimarisha benchi letu la ufundi kwa kuleta kocha msaidizi pamoja na wa makipa," alisema Mo Dewji.

KAZI IMEANZA...




Mshambuliaji mpya wa Azam FC, Mzimbabwe Prince Dube, akishangilia baada ya kuifungia timu hiyo bao pekee dakika ya 89 wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya KMC kwenye mchezo wa kirafiki uliopigwa katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Mdhamini aijaza Mbeya City mamilioni Ligi Kuu

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Mbeya City imepata mdhamini mpya baada ya Kampuni ya Parimatch inayojihusisha na michezo ya kubahatisha kuingia nayo mkataba wa mwaka mmoja wenye thamani ya Sh. milioni 270, imeelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, katika Ofisi za Shirikisho la Soka nchini (TFF), Mkurugenzi wa klabu hiyo, Emanuel Kimbe, alisema wamefarijika kupata udhamini huo na kuwataka wadau mbalimbali wazidi kujitokeza kuiunga mkono timu hiyo.

Mwenyekiti huyo alisema watazidi kujituma zaidi msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza wiki ijayo, ili kuwapa burudani mashabiki wao na kuwavutia wadhamini zaidi.

"Sisi kama Klabu ya Mbeya City, tumefarijika kupata mdhamini huyo, tunaamini tutazidi kutoa ushindani msimu ujao wakati Ligi Kuu itakapokuwa imeanza," alisema Kimbe.

Alisema wamejipanga kushika nafasi ya juu katika msimamo wa ligi hiyo ambayo inatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa.

"Timu yetu inaendelea na mazoezi kuelekea msimu ujao ambao tunaamini utakuwa na ushindani mkubwa tofauti na msimu uliopita," alisema.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa Kampuni ya Parimatch, Tumaini Maligana, alisema mkataba huo utakuwa wa msimu wa 2020/21 ambao utakuwa na faida kubwa katika klabu hiyo.

Alisema mbali na kuidhamini timu hiyo, wataendelea kuzidhamini klabu nyingine za chini kwa lengo la kukuza zaidi vipaji vya soka hapa nchini.

"Achilia mbali Mbeya City, bado tunafanya mazungumzo na klabu nyingine tutakazozidhamini ambazo kwa sasa mazungumzo na timu hizo yanaendelea," alisema Tumaini.

Aidha, aliipongeza Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) kwa kazi kubwa inayoifanya kuhakikisha soka la Tanzania linazidi kukua.

## Wasanii 50 ndani kampeni Mwana FA

**Na Steven William, MUHEZA**

KUNDI la wasanii nguli wa muziki nchini zaidi ya 50, wataunganisha nguvu pamoja kumpa sapoti mgombea Ubunge wa Jimbo la Muheza mkoani Tanga, Hamisi Mwinjuma maarufu Mwana FA katika uzinduzi wa kampeni Septemba 2, mwaka huu, imeelezwa.

Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi CCM Wilaya ya Muheza, Sufian Mwedi, jana alimwambia mwandishi wetu kuwa kundi la wasanii wakubwa na wadogo kutoka jijini Dar wakiongozwa na Ally Kiba watafika wilayani hapa kushusha 'shoo' ya nguvu katika uzinduzi wa kampeni ya mgombea ubunge huyo.

Alisema wasanii hao watawasili Muheza wakitokea jijini Dodoma kumuunga mkono mgombea Urais wa CCM, Rais John Magufuli kwenye uzinduzi wa kampeni za uchaguzi mkuu.

Mwedi alisema kwa upande wa Muheza, uzinduzi huo utafanyika katika Uwanja wa Jitegemee kwa wasanii mbalimbali kupanda jukwaani kabla ya Mwana FA kuanza kujinadi.

Alisema maandalizi ya uzinduzi huo yanaendelea kwa kasi wilayani hapa hiyo na kwamba siku hiyo shughuli rasmi zitaanza saa 12 asubuhi kwa maandamano ya miguu,pikipiki na magari kwa kupita mitaa mbalimbali ya mji wa Muheza wakiwa na mgombea ubunge na wasanii hao kuelekea Uwanja wa Jitegemee.

## JKU yamulika vifaa dirisha la usajili Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

ZIKIWA zimepita siku nane tangu kufunguliwa kwa pazia la usajili Ligi Kuu Zanzibar, timu ya JKU imesema imejipanga kusajili wachezaji wenye viwango vikubwa ili kuendana na kasi ya ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Omar Khamis Othaman, alisema bado hawajaweka wazi watasajili wachezaji wangapi ila nafasi wanazozipa kipaumbele katika usajili wao ni safu ya ushambuliaji, ulinzi pamoja na kiungo.

Alisema usajili wao utaangalia wachezaji kutoka madaraja tofauti yakiwamo Ligi Kuu, Daraja la Kwanza Kanda pamoja na Daraja la Pili Mikoa kwa kusajili wachezaji watakaotoa ushindani wa namba ndani ya kikosi na watakapokutana na wapinzani kwenye ligi.

"'Tunataka kusajili wachezaji watakaoweza kuisadia timu kufanya vizuri katika msimu wa 2020/21, maana Ligi ya Zanzibar hivi sasa ni ngumu sana tofauti na watu wanavyoiona, sisi malengo yetu ni kuwapata wachezaji wenye ushindani na uwezo mkubwa," alisema.

# Michezo

Jumamosi Agosti 29, 2020

Nipashe




HABARI UK 22

GRIEZMANN ATULIZWA

# REKODI KOCHA ZLATKO WA YANGA ZASHTUA

## ●●● Kutua leo, ana ubingwa wa CAF lakini timu 18 alizozinoa akidumu sana mwaka, huku...



Kocha Mkuu wa Yanga, Zlatko Krmpotic raia wa Yugoslavia, anayetarajiwa kutua nchini leo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE Klabu ya Yanga imemtangaza rasmi Zlatko Krmpotic raia wa Yugoslavia kuwa kocha mkuu wa timu hiyo akirithi mikoba ya Mbelgiji Luc Eymael baada ya Mrundi Cedric Kaze aliyekuwa akitarajiwa kuvaa viatu hivyo kukumbwa na matatizo ya kifamilia.

Jana Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM, Mhandisi Hersi Said, ambao wanaidhamini Klabu ya Yanga, alimtangaza Zlatko mwenye rekodi za kushtua katika klabu alizozifundisha kutokana na kuhama hata kabla ya mwaka kumalizika, kuwa ndiye atayerithi mikoba ya Eymael.

"Kocha atatua rasmi kesho na atakuwapo kwenye kilele cha Wiki ya Mwananchi Jumapili [Uwanja wa Mkapa], ni kocha mwenye uzoefu mkubwa na anafahamu vema mazingira ya Afrika, lakini pia amewahi kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Afrika akiwa na TP Mazembe (ya DR Congo)," alisema Hersi.

Hersi alisema tayari wamekubaliana na kocha huyo kutia saini mkataba wa miaka miwili na kwamba atakuwa akisaidiwa na mzawa Juma Mwambusi ambaye amepewa mkataba wa mwaka mmoja.

"Awali kabla ya Kaze kupatwa na matatizo ya kifamilia, alipendekeza kuwa na msaidizi mzawa, lakini pia alimtaka Kocha wa Makipa kutoka Burundi [Vladimir Niyonkuru], hivyo huyo tayari tumeingia mkataba naye kuwanoa makipa."

**Hata hivyo, pamoja na Hersi kueleza kuwa kocha huyo aliyetwaa ubingwa wa Afrika akiwa na TP Mazembe kama kocha msaidizi, kwamba amekubali mkataba wa miaka miwili kuinoa timu hiyo, hofu kubwa ni kumaliza kipindi hicho hasa kutokana na rekodi yake ya kutodumu kwa muda mrefu katika klabu moja.**

Katika klabu 19 alizozifundisha ni Degerfors IF ya Sweden pekee ambayo alidumu kwa kipindi kirefu kuanzia 1994–1996 na zingine 18 alizozinoa amekuwa akifanya kazi kwa mwaka mmoja ama pungufu ya hapo kabla ya kuachana nazo.

Beki huyo wa zamani wa Yugoslavia, Zlatko ambaye kwa sasa ana miaka 62, aliichezea timu hiyo ya taifa mechi nane kati ya mwaka 1980–1982 na timu yake ya kwanza kuinoa ilikuwa Degerfors IF kati ya mwaka 1994–1996, kisha akaifundisha loga Jugomagnat ya Macedonia, mwaka 1997–1998, kabla ya 1999 kuino Ankaragücü (Uturuki) na baada ya hapo mwaka 1999–2000 akatimkia OFK Beograd ya Serbia.

Mwaka 2000 akainoa Obilić ya Sebia kisha 2001 akaifundisha Paniliakos ya Ugiriki na mwaka huo huo akatimkia Nea Salamis ya Cyprus kabla 2002 kujiunga na Kairat ya Kazakhstan.

Mwaka 2005, Zlatko aliteuliwa kuwa Kocha wa U-17 wa Serbia and Montenegro na kipindi cha 2005–2006 akainoa Kazma ya Kuwaiti wakati 2007–2008 akirejea Serbia na kukinoa kikosi cha U-19.

Kituo kilichofuata kwa kocha huyo kilikuwa OFK Beograd ya Serbia akifanya kwa muda mfupi na kuondoka kisha mwaka 2014 akarejea tena kabla ya 2015 kuanza kufanya kazi Afrika kwa mara ya kwanza kwa kuwa kocha msaidizi wa Klabu ya TP Mazembe ya DR Congo.

Baada ya hapo kitua kilichofuata kwa kocha huyo kilikuwa Don Bosco ya Haiti mwaka 2016 kisha akarejea Afrika wakati huu akitua ZESCO United (Zambia) mwaka 2017 na mwaka uliofuata akatimkia Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Kituo kilichofuata kwa Zlatko kilikuwa APR FC ya Rwanda 2019 ambako mwaka huo huo akatimkia Polokwane City ya Afrika Kusini kabla ya sasa kujiunga na Yanga.

## SIMBA, MORRISON WAISIKILIZIA SERIKALI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba, umesema umepeleka maombi kwa mamlaka husika, Wizara ya Kazi kwa ajili ya kuwaombea vibali vya kufanya kazi nchini wachezaji wao wa kigeni akiwamo Mghana Bernard Morrison, ambaye amejiunga na klabu hiyo akiwa mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba na Yanga.

Mbali na Morrison nyota wengine wakigeni, ambao Simba imewaombea vibali ni pamoja na Mkenya Joash Onyango, Chris Mugalu (DR Congo) na Mzambia Rally Bwalya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Simba, Arnold Kashembe, alisema tayari wamefuata taratibu zote hivyo wanasubiri kujibiwa na wizara husika.

"Tumepeleka maombi yetu katika mamlaka husika ya kuomba vibali vya kazi kwa wachezaji wetu wa kigeni akiwamo Morrison, mchakato huo unaendelea," alisema Kashembe.

Naye Msemaji wa Idara ya uhamiaji, Paul John Mselle alisema wao wanatoa vibali vya makazi baada ya mhusika kupata kibali cha kazi.

Alipoulizwa Kamishna wa Kazi, Andrew Mwaluisi, alisema: "Tumepokea maombi mengi ila tusubiri Jumatatu tutajua."

Yanga bado inadai Morrison ni mchezaji wao, na imewasilisha rufaa Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya Masuala ya Michezo (CAS) ikipinga hatua ya TFF kumtangaza ni mchezaji huru.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >